# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Septemba 10, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581429

www.ippmedia.com





UKURASA 9


SUPA JACKPOT

TZS. 1,151,104,636

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Biteko aagiza Ardhi si wizara utatuzi migogoro

UKURASA 3


nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Askari polisi ajiua kwa risasi akilinda mitihani

UKURASA 2



Kinamama wa jamii ya Kimaasai, wakitoa adhabu ya bakora kwa wanawake wanaodaiwa kuhusika na ukiukwaji wa mila na utamaduni za jamii hiyo, kwa kujihusisha kimapenzi na watoto, wazazi wao au wakwe zao pamoja na makosa mengine ya kimaadili katika kijiji cha Orkeeswa, Monduli mkoani Arusha mwishoni mwa wiki. Kushoto ni kundi la wanawake wakisubiri adhabu hiyo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Tundu Lissu agonga mwamba, ahutubia mikutano kwa simu

UKURASA 3

UKURASA WA 4

### KASI MAENDELEO ILIVYOGEUKA KILIO KWA WANAFUNZI VYUO VIKUU

KASI ya maendeleo katika maeneo ya Mwenge, Survey...

UKURASA WA 3

### LESENI 45 KUTOLEWA UVUVI WA BAHARI KUU



SERIKALI imeingia mikataba itakayotoa leseni 45 za kuendesha shughuli za uvuvi...

UKURASA WA 17

### TETEMEKO ARDHI LAUA WATU 820

IDADI ya watu waliokufa katika tetemeko la ardhi nchini Morocco inazidi kupanda, mpaka jana jioni...



## DC azima jaribio ndoa ya mwanafunzi, mwanajeshi

UKURASA 2


MICHEZO YANGA: TUMEKWISHAFUNGA HESABU UK.24

KATUNI UK.6

# Askari ajiua kwa risasi akilinda mitihani la 7

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

ASKARI polisi, Koplo Petro Nyabucha, amejiua kwa kujipiga risasi shingoni akiwa chooni kwenye moja ya majengo ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Taarifa zinasema Koplo Nyambucha ambaye pia ni Mganga wa Zahanati ya Jeshi la Polisi katika Kikosi cha Kuzuia Ghasia (FFU) eneo la Mahenge, Manispaa ya Songea, siku ya tukio alikuwa akilinda mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, inayotarajiwa kuanza Jumatano ya wiki hii.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya washuhuda ambao hawakutana majina yao yaandikwe, walisema tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 1:00 asubuhi.

Kwa mujibu wa mashuhuda hao, Nyambucha alikuwa na askari wenzake waliokuwa wamepangwa kulinda mitihani ya darasa la saba inayosubiriwa kusambazwa wilayani.

Walisema Nyambucha aliondoka bila kuwaaga wenzake, ndipo wakaanza kumtafuta kwa kuwauliza baadhi ya watu waliokuwa karibu na eneo la jengo walilokuwa wakilinda mitihani hiyo.

Askari hao walisema wakati wanaendelea kumtafuta ndipo walimkuta chooni akiwa tayari amejiua kwa kujipiga risasi shingoni, jambo ambalo lilisababisha taharuki kwa watu waliokuwa jirani na eneo hilo.

Walisema baada ya kubaini tukio hilo kutokea, baadaye taarifa zilitolewa kwa viongozi wa eneo hilo na wa Jeshi la Polisi ambao walifika na kufanya taratibu za kumtafuta daktari ambaye alifika na kuthibitisha kuwa Nyambucha alifariki dunia kwa kujipiga risasi shingoni.

Baada ya kuthibitisha, mwili huo ulipelekwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma, mjini Songea huku taratibu za kuusafirisha mwili kwenda Ukerewe mkoani Mwanza zikifanyika.



Vizimba vikiwa wazi kwenye soko la kisasa lililopo karibu na kituo kikuu cha mabasi cha Magufuli, Mbezi Luis Dar es Salaam jana. Katibu wa soko hilo lenye uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 800, Joseph Shija (hayupo pichani) alisema wafanyabiashara wamelikimbia kutokana na kukosekana kwa wateja. **PICHA: SABATO KASIKA.**

# DC azima jaribio la ndoa kati ya mwanafunzi na mwanajeshi

**Na Vitus Audax,**
MISUNGWI

MKUU wa Wilaya ya Misungwi, Paul Chacha, amezuia kufungwa ndoa kati ya askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na mwanafunzi aliyemaliza kidato cha nne.

Askari huyo (jina halijafahamika) alitaka kumuoa binti huyo ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Mamaye, Misungwi mkoani Mwanza kwa kutoa mahari ya Sh. milioni 2.5

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya mkuu wa wilaya kufika katika familia hiyo, wazazi wa binti huyo walikiri kupokea mahari ya kutaka kumwozesha binti yao, wakisema walemazimika kufanya hivyo kwa sababu ya ugumu wa maisha.

Baba mzazi wa binti huyo, Pauline Malekela, alisema licha ya kuwa na ugumu wa maisha, pia msukumo wa binti yao uliwafanya kufikia uamuzi huo kwa sababu alikubali kuolewa na askari huyo na kumwambia alete posa nyumbani.

"Hatukumlazimisha kufanya hivyo bali walikutana huko, sisi huku akatushinikiza kuwa anaolewa na kutokana na sisi kutokuwa na fedha za kumudu mahitaji yake ya kwenda shuleni, tukakubaliana naye," alisema Malekela.

Mama mzazi wa binti huyo, Maria Daudi, licha ya kushukuru viongozi wa serikali waliozuia ndoa hiyo, aliomba binti yao asaidiwe mahitaji ya kwenda kuanza shule.

Alisema wanakiri kufanya kosa la kumwozesha binti yao, hivyo kuomba radhi na kuiomba serikali kuendelea kuwasimamia na kuhakikisha binti yao anapata elimu stahiki.

"Tutahakikisha sasa anatekeleza malengo yake ya kufika chuo kikuu. Lengo ni afanikishe malengo yake ya kielimu kwa ajili ya maisha yake ya baadaye,"alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Chacha, alisema alipata taarifa za binti huyo kutaka kukatishwa masomo, ndipo akachukua hatua za kuzuia tukio hilo. Kadhalika, alimtaka kijana aliyetaka kumuoa binti huyo kumlipia ada na kutoruhusiwa kufanya mawasiliano naye hadi pale atakapomaliza masomo yake.

Pia alimpatia binti huyo mahitaji yote muhimu ya shule kama vile godoro, sanduku la kuwekea vifaa vya shule, huku akibaki kwenye uangalizi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe ambako anakwenda kwa ajili ya masomo.

# Waziri Silaa aonya viongozi wanaogawa maeneo ya wazi

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ameanza kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kukagua eneo la wazi lililoko Mtaa wa Surungai, Meriwa Kata ya Ipagala mkoani Dodoma, huku akisisitiza maeneo ya wazi kuendelea kuwa wazi.

Katika ziara hiyo juzi, Waziri Silaa aliambatana na Kamishna wa Ardhi, Nathaniel Nhonge, watendaji wa sekta ya ardhi na watendaji wa kata ya Ipagala.

Akiwa eneo hilo, Silaa aliona baadhi ya wananchi walivyovamia eneo la wazi, huku baadhi yao wakiwa wamekamilisha ujenzi.

Baadhi ya viongozi wa mitaa wameidhinisha kuuza maeneo ya wazi kienyeji kinyume cha michoro ya mipango miji jambo lililosababisha ujenzi kufanyika, huku maeneo mengine ujenzi ukiendelea.

"Kama huu mchoro ungezingatiwa hapa pangekuwa na mji mzuri na eneo la wazi lingebaki. Wale wananchi wanaoishi na maeneo yao kuwekewa umeme wasibughudhiwe na simamieni maeneo yote yaliyobaki yabaki wazi hapa na maeneo mengine nchi nzima" alisema Waziri Silaa

Alisema kiongozi au mtendaji atakayebainika kusaidia wananchi kujenga eneo la wazi basi atawajibika kwa nafasi yake lakini kwa sasa pale wananchi walipojenga na kuishi, waendelee kuishi na wasibughudhiwe.

"Yale maeneo ya wazi ambayo yako wazi mtu anajenga kiukuta anaweka kibanda na yote yaliyokuwa wazi ama yenye uimarishaji wa muda mfupi au watu wamejitengenezea ukuta, yote yanatakiwa kuwa wazi " alisema Silaa.

Alisema akikuta maeneo ya wazi yamejengwa maana yake kiongozi au mtendaji aliyeruhusu kujengwa atakuwa sehemu ya mgogoro na atachukuliwa hatua huku akiwaonya maofisa wa sekta ya ardhi wanaomilikisha wananchi kiwanja kimoja mara mbili ambapo alieleza kuwa, ofisa atakayebainika atawajibika kwa kosa hilo.

Mwanzoni mwa wiki hii, Waziri Silaa alielekeza watendaji wa sekta ya ardhi nchini kuhakikisha ndani ya siku 100 kuanzia Septemba 4, mwaka huu, wanatatua migogoro ya ardhi kwa kadri ya uwezo wa nafasi zao.

Pia aliwataka waliovamia maeneo ya wazi kuanza kuondoka mara moja, huku akielekeza viongozi na watendaji wa Wizara ya Ardhi wenye mamlaka ya kusimamia sheria katika maeneo mbalimbali kuhakikisha ndani ya siku 1000 maeneo hayo yanakuwa wazi.

## Leseni 45 kutolewa uvuvi wa bahari kuu

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeingia mikataba itakayotoa leseni 45 za kuendesha shughuli za uvuvi katika bahari kuu ili kuleta tija na kuongeza mnyororo wa thamani katika uvuvi.

Hatua hiyo itaifanya sekta hiyo kuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi wa taifa.

Mikataba hiyo iliingiwa kati ya Mamlaka ya Usimamizi Uvuvi Bahari Kuu, Kampuni ya Albakora kutoka Hispania na Chama cha Wavuvi wa China.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam baada ya utiaji saini, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema mikataba hiyo ni moja ya manufaa ya mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF).

Alisema eneo la bahari kuu lina kilomita za mraba zaidi ya 220,000 ambazo zote ni mali ya Tanzania, akieleza kuwa bado hazijatumika ipasavyo.

Alisema serikali inaendelea kufanya ubunifu kuona ni namna gani bahari hiyo iweze kuwa na faida katika taifa.

"Uwezo wetu wa kutoa leseni ni zaidi ya leseni 100 kwa wakati mmoja na ili tupate faida zaidi ni lazima tuuze leseni kwa wingi, hivi sasa tumeanza kupokea baada ya kuondoa baadhi ya mambo kadhaa katika kanuni na kuboresha sheria zetu," alisema Ulega.

Alisema serikali imeanza kupokea wageni wengi wanaotaka kuchukua leseni za kufanya uvuvi katika bahari kuu na kati yao wapo ambao wamekuja kuunga mkono.

Aidha, alisema leseni hizo wanaziuza kwa Dola za Marekani, hivyo ni chanzo cha kupata fedha za kigeni, wakati wanaendelea na jitihada za kupata faida zaidi inayotokana na uchumi wa bahari, kama kujenga Bandari ya Kilwa Masoko, Zanzibar na Mangapwani.

Pia, alisema siku zijazo wanampango kujenga bandari ya mfano eneo la Bagamoyo na kwamba wanalenga samaki wavuliwe lakini wachakatwe hapa nchini ili kutoa faida ya kuendelea kuuza leseni, kutengeneza ajira, upatikanaji wa kodi na fursa mbalimbali.

Alisema hiyo pia itasaidia samaki kuandikwa 'made in Tanzania' (wametoka Tanzania) na kulipa taifa faida kubwa, huku akiwapongeza Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu.

Ulega alisema: "Hii ni mwanzo tuu lakini tunawataka mtafakari zaidi na msilale usingizi nchi inataka kuona namna ambavyo tunafanya ubunifu zaidi, bado manufaa ya bahari yanapaswa kuwa makubwa zaidi kuliko tulivyo leo.

"Fedha zitakazopatikana kwa mujibu wa sheria zetu ni kwamba asilimia 50 inabaki katika kazi za uendeshaji wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, asilimia 30 zinakuja Serikali ya Jamhuri ya Muungano na asilimia 20 zinabaki Serikali ya Mapinduzi Zanzibar".

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame, alishukuru kampuni hizo kwa kuja kuwekeza Tanzania, akieleza kuwa milango ya uwekezaji yako wazi na wanaendelea kuwaalika waje kuwekeza zaidi nchini.

Naibu Katibu wa Chama cha Wavuvi China, Chen Xuejian, aliahidi kuwa wataendelea kushirikiana na Tanzania ili kuongeza tija na kukuza sekta ya uvuvi.

# Lissu agonga mwamba, ahutubia kwa simu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MSAFARA wa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, jana ulizuiwa kuingia ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ili kufanya mkutano wa hadhara.

Eneo hilo ni lile ambalo kwa sasa serikali inaendelea na uhamasishaji wa wananchi waondoke kwenda Kijiji cha Msomera, Handeni mkoani Tanga, kwa lengo la kupisha shughuli ya uhifadhi.

Msafara wa kiongozi huyo ukiwa njiani kwenda eneo hilo, ulikumbana na kigingi kutoka Jeshi la Polisi wilayani Karatu, hali iliyowalazimu wafuasi wa chama hicho kupiga kambi barabarani.

Katika hali isiyo ya kawaida, baada ya msafara huo kuzuiwa, Lissu alianza kuhutubia kwa njia ya simu na mkononi wananchi waliokuwa wamekusanyika kumsubiri Ngorongoro.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Amani Golugwa, alisema Lissu alikuwa na ratiba ya kwenda kuhutubia eneo la Ngorongoro kwa kufanya mikutano mitatu ya hadhara Enduleni, Mamlaka na Nainokanoka.

Golugwa alisema alipotoka hotelini alikofikia Karatu Mjini, kabla ya kufika eneo la Changarawe, polisi walimzuia kupita barabarani.

"Polisi walisema Lissu hana kibali cha kwenda Ngorongoro lakini tulijaribu kuwaeleza wao si watoaji wa kibali kwa sababu tayari aliwasiliana na mamlaka na wakasema vibali vinapatikana pale geti kuu la kuingilia. Wakati msafara unakwenda hapo ukapate kibali, kabla ya kufika, polisi walizuia msafara wa Lissu na kusababisha malumbano," alisema.

Golugwa alisema mabishano hayo yalidumu muda mrefu, huku Lissu na wenzake wakikaa katikati ya barabara kusubiri kuruhusiwa kwenda Ngorongoro, hali iliyolazimu Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) ya Karatu na Askofu Maximilian Machimu kufika eneo hilo kushauriana naye ili kuondoka barabarani.

"Kweli baada ya mashauriano hayo, Lissu aliamuru msafara wake kurudi Karatu hotelini na huko alianza kuhutubia wananchi waliofurika kwenye mikutano katika maeneo hayo kwa simu," alisema.

Alisema leo ataendelea na mikutano yake wilayani Karatu kuzungumza na wananchi maeneo mbalimbali.

**KAULI YA LISSU**

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuzuiwa kufanya mkutano, Lissu alisema: "Wametupiga mabomu baada ya kuwa tumefunga barabara, wakatutawanya. Sasa ujumbe wangu kwenu ni kwamba tutakuja Ngorongoro.

" Bado tutakuja Ngorongoro. lazima tuje Ngorongoro kwa sababu si gereza, na nyie si wafungwa. Nyie ni raia wenye haki kama walivyo wengine. Tutapanga siku nyingine tutakuja Ngorongoro."

Lissu alisema katika msafara wake uliokuwa na magari matatu, mawili yalikatiwa vibali. Alisema msafara ulikuwa na watu 21 na kwamba 14 walipata vibali na ambao hawakuwa na vibali waliambiwa wangepata katika geti la kuingia katika Hifadhi ya Ngorongoro.

"Hakuna sheria ya nchi ambayo Jeshi la Polisi linatoa kibali cha kuingia katika Hifadhi ya Ngorongoro, hawana mamlaka wala haki ya kisheria ya kutuzuia," alisema Lissu.

Nipashe lilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, ili kupata ufafanuzi wa tukio hilo lakini alipopigiwa, simu yake haikupokewa.

Juzi, Mkuu wa Polisi Wilaya ya Ngorongoro, Peter Lusesa, alitoa barua ya kuzuiwa mikutano ya Lissu kutokana na sababu za kiusalama katika eneo la Loliondo na Ngorongoro.

Hata hivyo jana (juzi) Lissu alifanya mikutano Tarafa ya Loliondo katika Vijiji vya Ololosokwani na Wasso na jana alikuwa aendelee na mikutano Ngorongoro.



Babalishe Hamis Abdallah akisonga ugali, kwa ajili ya wateja wake katika eneo la Goba, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Biteko: Ardhi si wizara ya kutatua migogoro

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amemtaka Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kuifanya wizara hiyo kutekeleza majukumu yake ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi badala ya kuwa ya utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Aidha, ameagiza Kituo cha Taifa cha Ubunifu na Mafunzo ya teknolojia ya Taarifa za Kijiografia kitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na si kichaka cha kujipatia posho.

Dk. Biteko alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa kituo hicho jijini hapa.

"Nakuomba umeenda wizarani moja ya kazi ambazo unazo na Katibu Mkuu ni kupanga, kupima na kumilikisha na wewe umeeleza vizuri KKK tatu. Sasa tujipime na kujitathimini kama sekta yetu ya ardhi kazi hizi tunazifanya kwa ukamilifu wake.

"Lipo wimbi la kutokuwa au kuhamisha 'tension' ya wizara kuitoa kwenye majukumu yake muhimu yaliyotajwa kwenye sheria yake na kwenye ilani ya uchaguzi na kugeuka kuwa Wizara ya utatuzi wa migogoro ya ardhi,"alisema.

Alimtaka Waziri Silaa kubadilisha santuri na kuwafanya Watanzania wazungumze kuhusu mipango miji, maendeleo ya makazi na matumizi bora ya ardhi.

"Dodoma kwa mfano ni mji unaokuwa kwa kasi, tukifanya makosa hapa mwanzoni tukashindwa kuupanga sasa tukaruhusu kila aina ya ujenzi nataka niwaambie miaka ijayo vizazi vinavyokuja vitatushangaa, tunayo nafasi sasa ya kuipanga Dodoma kuwa makao makuu ya nchi ifanane na nchi zingine kubwa ambazo tunaweza kuzitembelea kwa sababu fursa hiyo tunayo na uwapo wa kituo hiki unaweza kutusaidia kufanya jambo hili.

"Wataalam wako, imarisheni ushirikiano na halmashauri. Haina maana yoyote huku wizarani unapanga mambo yako, halmashauri inapanga mambo yake mkija kuanza kutekeleza unakuta wizara inachosema na halmashauri inachosema haikutani mahali popote,"alisema.

Biteko aliagiza uondolewe urasimu kwa Watanzania na wale wanaostahili kupata hati wapate kwa wakati.

"Kama kuna migogoro na ukiona migogoro mingi inatokea haitokei kwa bahati mbaya kwa sababu kuna mtu mahali fulani hakutekeleza wajibu wake kwa wakati matokeo yake akaweka akiba ya migogoro ambayo tunatumia mamilioni ya pesa kufanya utatuzi wa migogoro.

"Twende tukaimarishe lakini tupange miji yetu, tuimarishe makazi ya watu tuijenge Tanzania iliyobora zaidi kuliko tuliyoikuta ili watoto wa watoto wetu wakija wakutikiwa bora na wao wajenge kuanzia hapo kujenga Tanzania iliyo bora zaidi," alisema.

Kuhusu kituo hicho, alisema kitakuwa kikubwa na kumwomba Waziri Silaa kukifanya kuwa cha kugombewa na Watanzania kujifunza.

"Itakuwa bahati mbaya sana watu wageuze kujifunza hapa kwa ajili ya kulipwa posho ya mafunzo. Kiwe kituo ambacho kitaongeza thamani na Mheshimiwa Waziri, wizara yako ni moyo wa shughuli zote za uchumi hapa nchini.

"Inahitaji msukumo mkubwa sekta yako ya ardhi,nikutie moyo waziri na watendaji wengine pamoja na kazi kubwa iliyofanyika ya kuimarisha sekta hii na amini na watanzania ni mashahidi bado tuna kazi ya kufanya,"alisema.

Waziri Silaa alisema kituo hicho kitatoa mafunzo na ushauri kuhusu ukusanyaji, uchakataji, uandaaji ramani za msingi za uwandani ambazo ni muhimu katika usanifu wa miundombinu ya miradi mbalimbali ambayo utekelezaji wake unahitaji ujuzi wa taarifa za kijiografia kama usafiri na usafirishaji, huduma za kijamii, umeme, maji, mafuta gesi na mawasiliano.

Alisema ardhi iliyopimwa kwa nchi nzima hadi sasa ni takribani asilimia 25 hivyo uwepo wa kituo hicho utasaidia kuboresha ujuzi wa watumishi na hivyo kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vya kisasa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO
MKOA WA MOROGORO

KATIKA SHAURI LA MADAI NA. 1/2023

NSHINBA SAN LIMITED: ..........................................MDAI

DHIDI YA

YONA T. MATEMBO: ..............................................MDAIWA

**WITO/KUITWA SHAURINI**
YONA T.MATEMBO

**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 29/09/2023 saa 2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.

Endapo hutofika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
**Imesainiwa leo tarehe 07 mwezi 09 mwaka 2023**

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MOROGORO.

RIPOTI MAALUM

# Kasi ya maendeleo ilivyogeuka kilio kwa wanafunzi wa vyuo vikuu



Sehemu ya muonekano wa mradi wa stendi mpya ya mabasi Mwenge katika Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana, ambao ujenzi wake unaelekea kukamilika. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**Na Waandishi Wetu**

KASI ya maendeleo katika maeneo ya Mwenge, Survey, Mlalakuwa na Lufungira wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, imesababisha kupaa kwa kodi za nyumba hali inayofanya maisha kuwa magumu kwa wakazi wengi, husus ani kwa wanafunzi.

Maeneo hayo kwa sasa kila uchao, mabadiliko makubwa ya majengo ya kisasa, miundombinu ya barabara za lami na majengo ya umma kama kituo kipya cha mabasi na kiwanja cha mpira cha timu ya soka ya KMC iliyo chini ya Manispaa ya Kinondoni yamekuwa yakionekana.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakazi wa maeneo hayo, wakiwamo wanafunzi, walisema kwa sasa bei za vyumba ziko juu tofauti na awali jambo linalowaumiza wenye kipato cha chini.

Walisema awali chumba cha kawaida (havina marumaru, dari ya kawaida na haina aluminium) vilikuwa Sh. 30,000 lakini kwa sasa imepanda hadi Sh. 50,000 kwa mwezi. Miundombinu ingali chakavu na chumba kizuri kodi yake ni Sh.80,000 kwa mwezi.

Mwanafunzi anayesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Zaituni Salehe, anayeishi maeneo hayo alisema, miundombinu ya vyumba na mazingira kiujumla haviendani na gharama wanazotoza wenye nyumba.

"Kodi iko juu sana, lakini vyumba tunavyokaa havina ubora kulinganishwa na gharama tunayolipa. Sakafu, dari na mazingira kwa ujumla ni chakavu sana. Hatuna uwezo wa kukaa kwenye vyumba vya bei kubwa," alisema Salehe.

Mwanafunzi mwingine anayesoma Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumain Dar es Salaam (TUDARCo), Jane Peter, alisema kodi zimepanda sana lakini mazingira ni mabovu, marekebisho ni hafifu na wakati huo huo mtu anatakiwa kumlipa dalali kodi ya mwezi kabla ya kuingia kwenye nyumba.

"Dalali anahitaji pesa ya mwezi mmoja kama malipo na hiyo ni tofauti na malipo kwa mwenye nyumba. Hata ukilipa kodi hizo, hawafanyi marekebisho kama wanavyoahidi," alisema.

Mwanafunzi mwingine, Raymond Ntenga, alisema licha ya vyumba kuwa ghali eneo hilo, sababu ya wao kuishi katika mazingira hayo ni eneo kuwa karibu na vyuo.

"Usafiri ni gharama na ukiishi mbali na eneo hili, utalazimika kutumia gharama nyingi zaidi kufika chuoni. Kwa hiyo hatuna budi kuishi katika mazingira haya kwa sababu hiyo," alisema Ntenga.

Paul Godfrey mkazi wa mtaa huo alitoa wito kwa wenye nyumba kuboresha vyumba, ili mtu anapolipa kodi kubwa iendane na chumba kama ilivyo kwa maeneo mengine.

Mmiliki wa nyumba eneo hilo, Eribaliki Mgodomi, alisema bei zimekuwa juu kutokana na changamoto ya wanafunzi kuharibu miundombinu ya nyumba wanazopanga pamoja na ujio wa kituo cha daladala na uwanja wa mpira.

Alisema shida iliyoko kwa wanafunzi anapanga mmoja lakini baada ya muda wanaishi watatu hadi watano ndani ya chumba kimoja, hali inayosababisha kuongezeka kwa matumizi ya vyoo, umeme na maji pamoja na kuchagiza uharibifu wa miundombinu. Alisema hiyo ndiyo sababu wanaongeza kodi.

> "Mwenge imezungukwa na vyuo vingi lakini vingi havina hosteli. Ninachoweza kushauri serikali ijenge hosteli kwa ajili ya wanafunzi ili kuwaepusha na gharama ya kupanga nyumba kwa bei kubwa na kuishi katika mazingira hatarishi.

### JICHO LA WACHUMI

Mchumi na mtaalamu wa masuala ya fedha katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Prof. Marcellina Chijoriga, alisema kupanda kwa bei ya vyumba kwenye eneo fulani kunatokana na uchache wa nyumba na ukuaji kibiashara kwenye eneo husika.

Alisema kwa sasa eneo la Mwenge limekuwa sehemu ya thamani kwa sababu ya ujio wa kituo kipya cha mabasi pamoja na uwanja wa mpira wa miguu.

"Maeneo ya Mwenge, kuna uhaba wa nyumba kwa sababu unapokuwa na wanunuzi wengi na bidhaa inayotolewa inapokuwa kidogo, lazima wanunuzi wataumia na wamiliki watafaidi. Eneo hilo lina nyumba na wahitaji ni wengi, hivyo lazima bei itapanda tu.

"Kuna athari kubwa kwa wanafunzi na wakazi wenye kipato cha chini hasa kodi ya pango inavyoongezeka. Nyumba ni kitu cha muhimu, mwanafunzi atakayeshindwa kupanga eneo hilo atalazimika kwenda mbali zaidi na chuo ukizingatia wengi zaidi wanategea hapo kwa sababu pamezungukwa na vyuo vingi.

"Wafanyabiashara wa kawaida watashindwa kumudu biashara na kuishi eneo hilo kwa hiyo watalazimika kuhama au kwenda eneo jingine kitu ambacho kitaathiri ukuaji wa uchumi wa nchi yetu," alisema mtaalamu huyo wa uchumi.

Mchumi mwingine kutoka Taasisi ya Uongozi na Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, alishauri serikali ijenge hosteli ili kuwaepusha wanafunzi kuishi kwenye nyumba za gharama kubwa ambazo haziendani na kipato chao.

"Mwenge imezungukwa na vyuo vingi lakini vingi havina hosteli. Ninachoweza kushauri serikali ijenge hosteli kwa ajili ya wanafunzi ili kuwaepusha na gharama ya kupanga nyumba kwa bei kubwa na kuishi katika mazingira hatarishi.

"Kwa wengine ambao si wanafunzi, mfano wafanyabiashara, hakuna namna inabidi watafute sehemu ambayo inaweza kuendana na kipato chao kwa sababu eneo la Mwenge kila siku linapanda thamani," alishauri Dk. Olomi

**Imeandikwa na Halfani Chusi, DAR, Antoni Manjoro na Julieth Ng'oma (TUDARCo)**

# Rais Samia kufungua mkutano wa vyama vya siasa

**Na Pilly Kigome**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufungua mkutano maalum wa Baraza la Vyama vya Siasa utakaowashirikisha wadau wa vyama vingi.



Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini ambae pia ni Mwenyekiti Kamati ya maandalizi mkutano huo, Mohamed Ali Ahmed, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam.

Ahmed alisema mkutano huo unatarajiwa kushirikisha zaidi ya wadau 500 kutoka kada mbalimbali zikiwamo taasisi za dini, mashirika, vyama vya siasa, vyama vya wenye ulemavu na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO).

" Tunapenda mtupelekee salamu juu ya mkutano huu maalum. Tunawakaribisha watu wa kada zote, waitikie kwa wingi kifika wakiwamo wananchi wajitokeze kutoa maoni na michango yao kuhusiana na demokrasia na hali ya vyama vingi nchini," alisema.

Ahmed alisema lengo la mkutano huo maalum ni kujadili na kupokea taarifa za kikosi kazi kilichoundwa mwaka 2021 na Rais Samia. Lengo lingine ni kujadili faida na changamoto zilizopatikana yakiwamo mapendekezo yaliyopatikana kwenye kikosi kazi hicho.

Mkutano huo, kwa mujibu wa Ahmad, utajadili hali ya siasa nchini, kutathmini wapi wametoka na wapi wanakwenda kupitia hali ya vyama vingi na demokrasia nchini.

Mkutano huo wa siku tatu unatarajiwa kuanza kesho katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) na utafungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

# Msonde ataja mwarobaini wa kukomesha ukatili kwa watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk.Charles Msonde, amesema ili kuhakikisha usalama wa watoto ni lazima kila shule kuwa na walimu wanasihi.

Walimu hao watakuwa maalum kwa ajili ya watoto kueleza vitendo mbalimbali vya ukatili wanavyofanyiwa wanapokuwa nyumbani, shule au njiani wakati wakienda shuleni na kurudi nyumbani.

Dk. Msonde aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo waratibu wa mpango wa shule salama na wasimamizi wa usalama wa jamii wa mikoa na halmashauri.

Alisema katika kutekeleza mpango wa shule salama ni lazima kila shule kuwa na mwalimu mnasihi ambaye watoto watamtumia kutoa kero ambazo wanakabiliwa nazo wakati wanapokuwa shuleni, nyumbani au njiani.

"Lazima shule kuwa na walimu wanasihi ambao watachaguliwa na wanafunzi wenyewe ambao watawatumia kueleza changamoto zao ili kulinda usalama wa mtoto," alisema.

Pia alisema ili kufanikisha mpango huo, kuna haja ya kuwa na mabaraza ya watoto ambayo watayatumia kueleza kero mbalimbali wanazokumbana nazo katika maeneo ya shuleni na nyumbani ili hatua zichukuliwe kabla hali haijawa mbaya.

"Lakini pia kuwapo kwa masanduku ya maoni katika shule ambayo watoto watatumia kueleza changamoto zinazowakabili na funguo za masanduku hayo lazima ziwe tatu moja kwa mwakilishi wa watoto, mwakilishi wa walimu na moja kwa wazazi," alisema.

Msonde pia aliwataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kushirikiana kikamilifu na walimu katika malezi na usalama wa watoto.

"Malezi na ulinzi wa mtoto ni jukumu letu sote, hivyo wazazi, walezi na jamii ishirikiane vyema na shule wasiwaachie tu walimu kwani mtoto anaweza kupata changamoto nyumbani, kwenye jamii ama shuleni. Ni muhimu kuwalinda kwa pamoja.

"Mwalimu anakuwa wa kwanza kabisa kumwona mtoto anapokuwa na changamoto kwa sababu watoto wengi wanakuwa wawazi na huru kuwaelezea walimu wao changamoto wanazozipitia hata kuliko ilivyo kwa wazazi wao," alisema Dk. Msonde

Ili kuboresha sekta ya elimu nchini, alisema serikali imekuja na miradi mbalimbali ikiwamo ya kuboresha Elimu ya Msingi na Sekondari na ule wa kuboresha Elimu ya awali na Msingi (BOOST).

Alisema katika mradi wa kuimarisha elimu ya sekondari (SEQUIP) serikali imewekeza Sh.trilioni 1.2 na mradi huo umekuwa ukisaidia katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika shule za sekondari.

"Kwa sasa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza wameongezeka na mradi wa SEQUIP umelenga kujenga shule 1,026 na katika shule hizo, 26 ni shule maalum kwa ajili ya wasichana na kila mkoa utajengwa shule moja," alisema.

Awali Mkurugenzi anayesimamia Elimu TAMISEMI, Vincent Kayombo, alisema maofisa 630 wanashiriki mafunzo hayo.

"Ni imani yangu kubwa kuona matokeo ya mafunzo haya yanakwenda kuleta tija katika shule na jamii kwa ujumla kila mmoja akatambue umuhimu wa malezi na ulinzi wa usalama wa watoto," alisisitiza

Alisema ongezeko la vitendo vya ukatili kwa wanafunzi vimesababisha shule kuwa si sehemu salama kwa wakati fulani, hivyo kutekelezwa kwa mradi wa SEQUIP na mafunzo hayo ya usalama, yamesaidia kwa kiwango kikubwa kurudisha imani ya wanafunzi, wazazi na walezi.




Meneja wa Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) Mkoa wa kikodi Ilala, Masau Malima (katikati), Meneja msaidizi huduma kwa mlipakodi, Penda Nkuba (wa nne kulia) na wafanyabiashara wakizindua kampeni ya "Tuwajibike" katika kituo cha huduma za kodi Gongolamboto, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yafadhili watumishi 500 masomo nje ya nchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali Awamu ya Kwanza 2023/24 umetoa ufadhili wa masomo ya muda mrefu na mfupi nje ya nchi kwa watumishi 500.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknoljia ya Habari, Mohammed Khamis Abdullah, alisema hayo jana jijini hapa wakati wa hafla ya kutoa vyeti vya ufadhili wa masomo ya muda mrefu nje ya nchi kupitia mradi huo.

Abdullah alisema katika ufadhili huo, watumishi 50 ndiyo watakaokwenda nje ya nchi kwa ajili ya masomo ya muda mrefu na wengine 450 ni masomo ya muda mfupi.

"Niwapongeze sana nyie ambao mmekuwa katika awamu hii ya kwanza ambao idadi yenu mpo 20 kati ya watu 211 walioomba nafasi za kushiriki mafunzo haya.

"Niwasihi huko mtakapokwenda kitu cha kwanza ni kutanguliza uzalendo wa taifa lenu na mtakachojifunza kule lazima mkilete nchini ili kuongeza tija katika masuala ya Teknolijia ya Habari na Mawasiliano," alisema.

Alisema ufadhili huo ni matokeo ya dhana ya serikali ya kukuza na kuimarisha rasilimali watu ili taifa kwenda katika dunia ya kidijitali.

Kadhalika, alisema kupitia mradi huo serikali imepanga kujenga vyuo viwili vya TEHAMA katika mikoa ya Dodoma na Kigoma pamoja na vituo vinane vya ubunifu.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Ulaya na Amerika katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Gerald Mbwafu, aliwataka watumishi hao walipata nafasi ya masomo nje ya nchi kuzingati sheria za nchi na vyuo wanavyokwenda kusoma.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Mrope, alisema serikali itahitaji kuwatumia watumishi hao kwa manufaa ya taifa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko mifumo ya kifedha kwa kilimo Afrika yaanzie ndani

**TANZANIA** wiki hii ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa 13 wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula (AGRF) uliofanyika Dar es Salaam kwa siku tano kuanzia Septemba 4, mwaka huu. Mkutano huo ulioshirikisha wakuu wa nchi na viongozi waandamizi wa serikali barani Afrika na washirika wa maendeleo ulijadili masuala mbalimbali juu ya kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo.

Suala hilo la mapinduzi ya kilimo lilipewa kipaumbele kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo sekta hiyo kuwa ndiye mwajiri mkubwa kwa nchi za Afrika, Tanzania ikiwamo. Kilimo pia ni chanzo cha maendeleo ya sekta ya viwanda kutokana na ukweli kwamba bidhaa nyingi za viwandani zinategemea bidhaa zinazotokana na kilimo.

Kutokana na umuhimu huo wa kilimo kwa maendeleo endelevu hasa kwa nchi zinazoendelea, mawaziri wa kilimo Afrika katika maazimio yao, walitoa rai kwa washirika wa maendeleo kurekebisha mifumo ya fedha ili kuiwezesha Afrika kunufaika na rasilimali zake na zile zilizoko duniani kwa ujumla.

Katika maazimio hayo, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema pamoja na mambo mengine, wamekubaliana kutafuta fedha kwa ajili ya mifumo ya chakula na baadhi ya taasisi ikiwamo Benki ya Dunia zimeahidi kusaidia katika eneo hilo. Kubwa zaidi, mawaziri hao waliazimia kwamba nchi wahisani na washirika wa maendeleo warekebishe mashrti ya upatikanaji wa fedha hizo ili kuwezesha Afrika kutimiza azma ya kunufaika na kilimo hatimaye kupiga hatua za kimaendeleo.

Ni dhahiri kwamba kwa kufanya hivyo, Afrika itajinasua katika umaskini kwa kuwa asilimia 65 ya rasilimali ambazo hazijatumika ziko Afrika. Kwa maana hiyo, iwapo masharti yatalegezwa kuhusu upatikanaji wa fedha, kutakuwa na mitaji mingi itakayowezesha nchi za Afrika kutumia rasilimali hizo, zikiwamo za kilimo na mifugo kupiga hatua za kimaendeleo.

Pamoja na kuziomba nchi za viwanda na washirika wa maendeleo kufanya hivyo, Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, wakati wa kufunga mkutano huo, alitoa rai kwa viongozi wa ngazi zote kuhakikisha suala hilo linatimizwa. Kwa maneno mengine, Dk. Biteko alihamasisha upatikanaji wa fedha hizo uanze ndani ya mataifa ya Afrika kabla ya kwenda nje.


Kuna msemo kwamba kilio huanza na mfiwa. Huo ni ukweli kwamba utatuzi wa tatizo ni lazima uanze na mhusika kabla ya kuomba msaada nje. Kwa mantiki hiyo, mipango ya kutafuta mitaji kwa ajili ya kuimarisha sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ambazo ndizo mhimili wa kuondoa umaskini na kukuza uchumi, ni lazima ianzie ndani.

Jambo la msingi na la msisitizo hapa ni kujenga uwezo wa ndani kwa kuongeza bajeti katika sekta hizo pamoja na kutunga sheria ambazo zitazibana taasisi za fedha za ndani katika kurahisisha upatikanaji wa fedha za mikopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo, mifugo na uvuvi.

Serikali inapaswa kujiuliza kama kuna mazingira rafiki ya upatikanaji wa fedha kutoka ndani kwa ajili ya maendeleo endelevu ya sekta zilizokuwa kiini cha AGRF. Pia hakuna budi kujiuliza kama riba zinazotolewa na benki kwa ajili ya mikopo hususan kwa kilimo na ufugaji kama ni rafiki na haziwaumizi wahusika.

Kwa jumla ni vigumu kuwataka washirika wa maendeleo, zikiwamo taasisi kubwa za kifedha zilizoko nje ya nchi, kupunguza riba na kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa fedha wakati mazingira ya ndani hayatoi nafasi katika kuleta unafuu. Mpango huu uanzie ndani ndipo utoke nje ya mipaka na hapo ndipo mafanikio ya kweli yatakapopatikana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Ulinzi na usalama wa waandishi upewe kipaumbele

**WAANDISHI** wa habari wanafanya kazi ya kuelimisha, kuhabarisha na wakati mwingine kuburudisha umma kupitia kalamu zao. Huo ndio wajibu wao wa msingi wa kitaaluma.

Taaluma inawapa majukumu hayo kwa jamii na wanapohabarisha, kuburudisha, kuelimisha huwa hawaingii kwenye msigano wowote na ama serikali au watu binafsi kwa kuwa wengi hufurahia kazi zao.

Lakini mara nyingi, waandishi hawa wanapotumia kalamu zao kufanya uchunguzi na kufichua maovu, iwe ni serikalini, taasisi za umma, binafsi na kwa mtu mmoja mmoja, wamekuwa wakionekana maadui na wakati mwingine maisha yao kuwa hatarini.

Mara nyingi umma unapenda kusoma habari zinazofichua wizi, ubadhirifu, ufisadi wa baadhi ya viongozi wawe wa serikali au kwenye taasisi yoyote ya umma na binafsi kwa kuwa ndizo habari pendwa kwao.

Lakini wakati wananchi wakifurahia habari hizo, kwa waandishi wanaofanya uchunguzi na kufichua habari hizo usalama wao huwa shakani. Wahusika wa wizi huo huanza kuwawinda wakati mwingine kutaka kuwanyamanzisha kwa njia mbalimbali.

Mwandishi anaweza kunyamazishwa kwa njia yoyote ikiwamo ya kurubuniwa kupewa rushwa, kutishiwa maisha, kuuawa au kutengenezewa mazingira yoyote ya hofu kuhakikisha anaachana kabisa na kufuatilia habari anayoifuatilia.

Waandishi wanawake wanakuwa kwenye hatari zaidi kulinganisha na wanaume wakati wa kuripoti habari za uchunguzi zinazofichua maovu kwenye jamii, hivyo kuna haja ya kuweka mifumo ya kuwalinda zikiwamo sheria ili kuwapa uhuru mpana wa kufanya kazi zao kwa amani.

Uzoefu unaonyesha kuwa baadhi ya waandishi hususan wanawake hupokea hata vitisho wanapoandika habari zinazofichua maovu yanayofanyika kwenye taasisi au ya mtu mmoja aliyefanya ufisadi na kusababisha hasara kwa serikali au kwa taasisi binafsi.

Ndiyo sababu tunaona kuna umuhimu kukawa na mifumo thabiti ya kuwalinda waandishi wa habari wanawake na wanaume kwa kuwawekea bima ya majanga ili wanapopata shida wakati wa kufanya habari zao angalau wapate unafuu wa maisha yakiwemo matibabu.

Habari za uchunguzi, uchunguzi unaonyesha ndizo mara kadhaa zimekuwa zikiwaingiza waandishi wa habari matatani kwani zimekuwa zikifichua uzembe, wizi na ufisadi wa baadhi ya viongozi kwenye maeneo yao ya kazi na kwa kuwa hawapendi habari hizo ziandikwe ni dhahiri mwandishi husika anaweza kujikuta yuko hatarini kupata madhara.

Ndiyo sababu tunaona kuna umuhimu wa waandishi wa habari kuwekewa sheria rafiki ambazo zitawasaidia iwapo watapata majanga wakati wakitekeleza majukumu yao ya kuhabarisha jamii kwa habari mbalimbali zikiwemo za uchunguzi.

Pamoja na kutaka kuwapo sheria rafiki zitakazowafanya waandishi wafanye kazi zao kwa furaha bila woga, kuna umuhimu pia wa kuwapa elimu ya namna ya kukwepa hatari wanapofanya habari za uchunguzi ili wanapokuwa kwenye maeneo ya kazi, wajue namna ya kujilinda.

Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 iliweka vifungu vyenye changamoto kubwa na vyenye ukakasi katika kumwezesha mwandishi wa habari kutekeleza majukumu yake bila woga.

Vifungu vyenye utata vipo vingi pamoja na kile kinachoweka adhabu kwa makosa ambayo hayako wazi kinyume cha Ibara 13 (6) (c), kufifisha uhuru wa kupokea na kusambaza habari kinyume cha Ibara 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wadau wa habari wanapiga kelele kuhusiana na kuwepo kwa baadhi ya vipengele ambavyo vimeonekana kuminya uhuru wa waandishi wa habari kutimiza majukumu yao ya kuhabarisha jamii na kukwamisha haki za upatikanaji habari.

Kuna baadhi ya vifungu vinaingilia haki ya kupata taarifa kama ilivyoelezwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mikataba ya Haki za Binadamu iliyoridhiwa au kusainiwa na Tanzania.

Vipengele vinavyolalamikiwa vimo kwenye sheria hiyo na Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta (EPOCA) ya mwaka 2010 ambayo inasimamia radio, TV na mitandao ya kijamii.

Pia Sheria ya Haki ya Kupata Habari ya mwaka 2016 na Sheria ya Makosa ya Mtandao ya 2015 zikiwamo kanuni za maudhui mtandaoni za mwaka 2018 zilizogawanywa katika vipengele mbalimbali, ni miongoni mwa maeneo ya vipaumbele ambavyo wadau wa habari wanataka maboresho ili kuongeza ufanisi kwa waandishi wa habari kutokana na kuwa na udhaifu na upungufu wa sheria.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Kwa nini Bunge haliondoi ubatili kwenye Katiba na sheria zetu?



Pascal Mayalla

LEO naendelea na sehemu nyingine ya Ijue Katiba ya JMT kwa jicho la mtunga katiba. Sehemu ya kwanza nilifundisha Katiba ni nini na ni ya nani. Sehemu ya pili, nilizungumzia mtunga Katiba alimaanisha nini aliposema Katiba ni Sheria Mama.

Katika mfululizo huu wa elimu kwa umma kuhusu Katiba, nawaletea mifano ya sheria batili inayokwenda kinyume cha katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) kwa kuonyesha Katiba inasema nini na sheria hiyo inasema nini. Mwisho nitaonyesha sheria hiyo batili imekinzana wapi na Katiba ya JMT.

Hata hivyo, ieleweke kwamba si mara ya kwanza kwa Bunge kutunga sheria batili lakini cha kujiuliza Watanzania tutaendelea kusubiri mpaka lini Bunge likitunga sheria batili na kuuchomekea ubatili huo ndani ya Katiba yetu?

Kwanza, tuanze na Ibara ya 5 ya Katiba ya JMT. Ibara hii inasema haki hii ndiyo haki kuu ya kwanza ya kidemokrasia, haki ya kupiga kura. Japo haki hii bado iko kwenye Katiba yetu, imeingiliwa na kukiukwa na ukosekanaji wa haki ya kuchaguliwa, hivyo Watanzania kuruhusiwa kuwachagua si viongozi wao wanaowapenda kwa uhuru, bali viongozi waliopitishwa na kundi fulani (kudhaminiwa na chama cha siasa). Kwa kufanya hivyo, ni kukiuka nia njema ya mtunga Katiba ya kila Mtanzania anakuwa na haki ya kupiga kura kuchagua kiongozi anayemtaka. Kwa Tanzania ni kumchagua kiongozi chama kilichowachagulia!

Pili, Ibara ya 5 (2) inalipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria kuzuia mtu kupiga kura.

Haki hii ya uhuru wa kupiga kura kuchagua ni moja ya haki zinazoitwa 'fundamental rights', yaani haki za msingi za binadamu.

Tatu, Ibara ya 3 imelipa Bunge la JMT mamlaka ya kutunga sheria ya uchaguzi.

Mamlaka haya ya Bunge kutunga sheria ya uchaguzi pia limewekewa masharti, hivyo Bunge halina mamlaka ya kutunga sheria inayokwenda kinyume cha Katiba.

Baada ya ibara hizo, tuangalie Ibara ya 21, Ibara ya 39 na Ibara ya Katiba ya JMT. Ibara ya 21 yha Katiba ya JMT inatoa haki ya kila Mtanzania mwenye sifa, kuwa huru kushiriki katika siasa na uongozi kuanzia serikali za mtaa hadi serikali kuu bila ubaguzi wowote.

Uhuru wa kwanza kabisa ni wa kushiriki shughuli za umma. Ibara ya 21 (1) inasema: "Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 5 ya Katiba hii na ya sheria za nchi kuhusiana na masharti ya kuchagua na kuchaguliwa, au kuteua na kuteuliwa kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria.

Lakini kukafanyika jambo kwa maslahi ya watu fulani, na kwa vile serikali ni yao, wakaipindua Katiba kwa kuinyofoa haki hiyo ya kila mtu kushiriki siasa, iliyotolewa na katiba na kupachika sharti la kudhaminiwa na chama. Hatua hiyo imesababisha kujenga ubaguzi katika kushiriki shughuli za uongozi wa umma kwa watu kulazimishwa kwanza kujiunga na vyama vya siasa ndipo upate haki ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi wa umma.

Huku si kuwatendea haki Watanzania wengine wote, wasiotaka kujiunga na vyama vyovyote vya siasa kutokana na kuviona karibu vyote ni vyama vya hovyo hovyo, lakini wana uwezo wa uongozi.

Hii ni haki muhimu iliyotolewa na Katiba. Kitendo cha kuingiza shurti la kudhaminiwa na chama cha siasa ni kinyume cha Katiba. Sheria hii ibadilishwe ili kukidhi kile ambacho Katiba ilidhamiria ilipoitoa haki hii.

Baada ya mabadiliko hayo ya mlango wa nyuma, kipengele hicho sasa kinasomeka hivi:

"Uhuru wa kushiriki shughuli za umma Sheria ya 1984 Na.15 ib.6 Sheria ya 1994 Na.34 ya Ibara ya 4, Ibara ya 21.(1) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 5, ya 39 na ya 67 ya Katiba hii na ya sheria za nchi kuhusiana na masharti ya kuchagua na kuchaguliwa, au kuteua na kuteuliwa kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria."

Ule uhuru uliotolewa na Katiba wa kila mtu kuwa huru kushiriki shughuli za uongozi, kupitia ibara ya 21, umekuja kunyofolewa na ibara ya 39 na ya 67 (b) (c) kwa kuweka sharti ili mtu kugombea nafasi yoyote ya uongozi wa umma, ni lazima awe mwanachama, na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa, hivyo lazima adhaminiwe na chama cha siasa!, Haki zinatolewa na ibara moja halafu zinaporwa na ibara nyingine ya katiba hiyo hiyo!

Mchungaji Christopher Mtikila (Mungu amweke mahala pema peponi) mwaka 1993, alifungua kesi No. 5 ya 1993 akifanya juhudi kubwa kukipinga kifungu hiki na Mahakama Kuu kupitia kwa Jaji Kahwa Lugakingira (Mungu amuweke mahala pema peponi), ikatamka wazi na bayana kipengele hicho ni batili na kinakiuka Katiba ya JMT ya mwaka 1977, hivyo kifutwe, na kutoa haki kwa kila Mtanzania ana haki ya kushiriki kugombea uongozi.

Baada tu ya Mtikila kushinda kesi, serikali ilifanya mambo mawili makubwa ya ajabu! Kwanza, ilikata rufani. Hivi kwa uamuzi kama huu, serikali ilikata rufani kwa maslahi ya nani? Pili, serikali ilipeleka bungeni kwa hati ya dharura, Sheria No. 34 ya mwaka 1994, kufanya marekebisho ya Nane ya Katiba ya JMT na kukichomeka kipengele hicho ndani ya Katiba, hivyo kuibatilisha ile hukumu ya Jaji Lugakingira!

Hapo ndipo ujinga unapoanzia katika siasa zetu kwa serikali kufanya kazi kwa maslahi ya kisiasa ya watu fulani, hivyo kupoteza haki ya wengi kwa ajili ya kuwanufaisha wachache. **Tukutane Jumapili ijayo...**

**PASKALI**
**+255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Nilichojifunza nikiwa mgeni wa Spika bungeni



Na Joseph Kulangwa

KUNA mambo mtu ukipata kuyafanya inabidi uwashukuru waliokuleta duniani, yaani wazazi wako. Hebu fikiria eti nami juzikati hapa nilikuwa miongoni mwa watu walioalikwa bungeni na Spika, Dk Tulia Ackson.

Eti nami siku hiyo kwa mshangao wa wengi nikajikuta ndani ya suti na tai ndefu kama ulimi wa kinyonga, nimetulia kwenye eneo ndani ya Bunge nikitambulishwa na Spika nikiwa mmoja wa wageni wake! Dunia ina mambo kwa kweli.

Mwenzangu mmoja, aliyebahatika kukaa karibu nami, naye nikamwona akiwa anashangaashangaa kila kitu alichokiona ndani ya ukumbi ule nadhifu, uliopambwa kwa rangi nyekundu za viti na zuria la rangi za Bendera ya Taifa.

Mshangao wake haukuwa mbali na niliokuwa nao mimi lakini kikubwa ni kuona viti vingi vikiwa tupu na wachache waliokuwamo, wengi wakichati na simu zao na wengine kusogoa. Nikajisema, angalau nimeamini nilichokuwa nikiambiwa kuwa kuna baadhi ya waheshimiwa si watoro lakini hutoroka mara moja moja.

Mara nikasikia Spika, mwenyeji wetu, akisimamisha mijadala na kuwataka wabunge kuongea kwa sauti za chini kwani za juu zilikuwa zinavuruga majadiliano ya muswada husika na kuwaambia kama wana jambo, milango ya jengo lile iko sita.

Awali nikidhani kuwa waheshimiwa wakiwa humo huwa watulivu wakisikiliza nini kinasemwa lakini kumbe la hasha, unaona kila mmoja ana lake jambo, mara huyu ahame kiti aende kule, mwingine atoke nje akazungumze na wapigakura.

Lakini baadaye akili ikanijia kwamba hawa si wanafunzi na wala si wafungwa, wana haki ya kufanya lolote ilimradi wanatuwakilisha na wanawakilisha mawazo na matakwa yetu sisi waajiri wao.

Nikajifunza mengi katika saa hizo chache nilizokalia kiti chekundu mjengoni kwamba kumbe kila mheshimiwa akiingia humo, anakuwa na letu lakini pia na lake, hasa pale mwenyeji wetu alipotutambulisha sisi wageni wake.

Hapo kumbuka alishatambulisha wageni wengine kibao, wakiwamo wa kwake wengine lakini pia wa wabunge wengine. Siku hiyo ya Alhamisi, siku moja kabla ya mkutano huo wa Bunge kuahirishwa, hakika ilikuwa siku ya wageni.

Sikutaka sana kulaumu nini walichokuwa wakifanya wabunge hasa kwa kutotulia vitini, nikijua kuwa siku hazigandi. Uchaguzi unakuja, ndiyo sababu wanaitwa wapiga kura kuja kutambulishwa bungeni hata kama alikuwa nao jana.

Jambo lingine lililonifurahisha na ambalo siku zote nilikuwa najiuliza ni kwa nini, ni lile la mbunge kusimama akauliza swali lake au kuomba swali lake lijibiwe, Naibu Waziri akasimama kulijibu, akasimama mbunge na kushukuru kwa majibu mazuri lakini ana swali la nyongeza.

Nikijiuliza hivi kama majibu ni mazuri, swali la nyongeza linatoka wapi? Na tena mheshimiwa mwuliza swali anaweza akakakamaa mpaka akasimama waziri mwenyewe mwenye dhamana ya swali lililokolenga, akajibu na ikishindikana atasimama Waziri Mkuu.

Lingine sasa ni hili la mheshimiwa kusimama, lakini badala ya kwenda moja kwa moja kwenye swali au mchango, ataanza kusifia Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na baraza zima la mawaziri kabla ya kuanza alichokipanga.

Ukijiuliza sana kwa nini aanze hivyo, utapata jibu tu bila shaka ni kwamba masanduku ya kura kivi sasa yanaanza kufutwafutwa vumbi kwa ajili ya mwakani na mwaka unaofuata, kwenye alichosema Chifu Hangaya kuwa ni kivumbi.

Kwa yote haya na mengine, kwa kweli nawapongeza waheshimiwa wabunge kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutuwakilisha sisi, kwani bila wao isingewezekana sisi sote zaidi ya watu milioni 60 kama tungetosha pale Dodoma, kuzungumza ya kwetu.

Lakini jambo langu la msingi mimi na wenzangu wachache wenye akili za hivihivi kama hizi, ni kutunza muda na wakati, lakini pia kuutumia vizuri kwa maslahi mapana ya wapiga kura na Taifa hili kwa ujumla, na ili tushuhudie thamani ya kweli ya pesa tunazolipana.

Hivi kwa nini mbunge utoke jimboni uende mkutanoni Dodoma, lakini unaonekana mara mbili au tatu tu tena bila Spika kujua, unafanya mambo yako nje ya Bunge! Hivi kweli kuna sababu ya kila mtu kupelekwa bungeni na kusimamisha muda wa Bunge ili kutambulishwa?

Kuna haja gani kwa muda mwigi wa Bunge kutumiwa na wabunge walioko ndani kuchati kwa simu janja na wengine kusogoa na kumwacha Spika na msemaji peke yao wakifuatilia? Zamani pale Karimjee hakukuwa na simu janja, hivi leo zipo watu watakwambia tunawasiliana na wapiga kura.

Nashauri hili tuliangalie sana, ili muda wa Bunge utumike kufanya ya wananchi, badala ya maslahi binafsi ya sanduku la kura! Watambulishwe wageni wa Bunge si wa wabunge mmoja mmoja. Mathalan kuna wabunge kutoka Bunge la nje na wengineo wa hadhi hiyo.

Waheshimiwa wabunge wakae bungeni muda wote isipokuwa kwa dharura, kwani ndicho tulichowachagulia na kuwatuma kufanya Dodoma, ili masuala ya wananchi yapewe kipaumbele na haki stahiki. Ila kila la heri kwa kazi ngumu na nzito waheshimiwa wabunge na ahsante Daktari Tulia kwa mwaliko. Alamsiki!

# Watumishi wa TANESCO waendelea kusota rumande

**Na Remmy Moka,**
SAUT

WATUMISHI wawili wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, wanaokabiliwa na mashtaka 125 ya uhujumu uchumi ikiwamo kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni mbili, wameendelea kusota mahabusu.

Hali hiyo inatokana na kesi yao kuahirishwa kutokana na hakimu anayesimamia kesi hiyo kuwa na udhuru.

Watuhumiwa hao, fundi mchundo Abdukadri Lwassa (39) na Ofisa Bohari wa TANESCO, Respicius Rwegoshora (33), juzi walifikishwa kwa mara nyingine katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza kusikiliza kesi yao namba 5/2023 ikiwa na makosa 125 yakiwamo kughushi nyaraka za serikali, ubadhirifu wa mali za umma na kutoa nyaraka za uongo.

Shauri hilo lilisikilizwa juzi mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Ilemela, Fotunatus Kubaja, na kuahirishwa kwa kile alichokieleza kuwa Hakimu Mkazi Mwandamizi Stella Kiama, anayesimamia kesi hiyo kuanzia mwanzo kapata udhuru.

**Hali hiyo inatokana na kesi yao kuahirishwa kutokana na hakimu anayesimamia kesi hiyo kuwa na udhuru.**

Hata hivyo, mwendesha mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Maximilian Kyabona, aliiambia mahakama kuwa bado wanaendelea na upelelezi, hivyo kuomba hakimu kupanga tarehe ya kusikilizwa tena kwa shauri hilo.

Hakimu Mkazi Kubaja aliahirisha kesi hiyo na kuamuru watumishi kuendelea kubaki rumande mpaka Septemba 13, kesi yao itakapotajwa.




Mkurugenzi wa Chama cha wataalamu wa Masoko Tanzania, Dk. Emmanuel Chao (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza Tuzo za Masoko na Kongamano la 2023 linalotarajiwa kufanyika Oktoba 27 mwaka huu kwenye ukumbi wa Blue Saphire. Wengine ni wadhamini wa tuzo hizo, Mwakilishi kutoka kampuni ya Bramex, Sylvia Joseph (kushoto), Gloria Malikita (kulia) na Iche Omari kutoka kampuni ya Smartcodes. P**ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sekta binafsi waitwa kuwekeza kwenye mbegu

**Na Renatha Msungu**

WAKALA wa Mbegu za Kilimo (ASA), imezitaka sekta binafsi kutumia fursa ya ushirikiano wa uzalishaji mbegu bora za mazao iliyotolewa na serikali ili kuongeza uzalishaji ifikapo mwaka 2025.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa ASA, Dk. Sofia Kashenge, wakati akielezea mikakati waliyojiwekea ili kuhakikisha wanafikia malengo ya serikali ya uzalishaji wa mbegu asilimia 75 ifikapo mwaka 2025.

Dk. Kashenge alisema hivi sasa serikali imewekeza katika kilimo, hivyo wawekezaji wazawa hususani vijana wenye kampuni za kuzalisha mbegu wanapaswa kujitokeza kwa wingi kuomba mashamba ya serikali yaliyoboreshwa kwa ajili ya kuzalisha mbegu.

"Wawekezaji wazawa wa kampuni za uzalishaji mbegu mjitokeze kwa wingi kushirikiana na serikali kuzalisha mbegu, tunahitaji kuona tunafikia malengo tuliyojiwekea," alisema Dk. Kashenge.

Alisema wamejiwekea mikakati ili kufikia azma ya Rais Samia Suluhu Hassan katika suala la uwepo wa mbegu za kutosha ifikapo mwaka 2025 ikiwamo kushirikiana na sekta binafsi katika uzalishaji.

Akizungumzia kuhusu suala la upimaji afya ya udongo, alisema wamejipanga katika mashamba ya serikali ambayo yanaboreshwa miundombinu yake yatapimwa afya ya udongo kabla ya kuanza kutumika.

Alisema wanafanya hivyo kwa sababu wanahitaji uzalishaji bora wenye tija, ambao utaliletea taifa manufaa makubwa ikiwemo kupunguza gharama za uagizaji mbegu.

"Suala la upimaji afya ya udongo ni la lazima, kwa sababu ili uzalishe kwa wingi ni lazima ujue afya ya udongo, ambayo itakuwezesha wewe kujua ni aina gani ya mazao yanayopaswa kulimwa katika eneo hilo,"alisema.

Alisema watahakikisha kila shamba linapimwa afya ya udongo na wataalam kutoka sekta ya kilimo ili kuhakikisha wanafikia malengo waliyokusudia.

Kutokana na hilo, aliwataka vijana kushawishika kuingia kwenye kilimo kwa sababu ni sekta kubwa.

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan alisema ifikapo mwaka 2025, taifa linatakiwa kuzalisha asilimia 75 ya mbegu bora ambazo zitakidhi mahitaji ya wakulima hapa nchini.

Kutokana na hilo, ndiyo maana serikali imewekeza katika kilimo biashara ambacho kinaleta manufaa kwa wakulima pamoja na taifa.

# TBS yaelimisha 2,276 kuhusu ubora bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetoa elimu kwa wananchi 2,276 kupitia kampeni yake ya kutoa elimu kwa umma katika wilaya za Malinyi, Ulanga, Gairo na Mvomero mkoani Morogoro kuhusu umuhimu wa kusoma taarifa zilizomo katika bidhaa.

Elimu hiyo pia inahusu watu kununua bidhaa zilizothibitishwa na shirika hilo sambamba na kuwahamasisha wajasiriamali wadogo kuthibitisha ubora wa bidhaa zao na wafanyabiashara kusajili maduka ya chakula na vipodozi.

Kampeni hiyo ambayo ilianza Agosti 21 na kumalizika Septemba 5, mwaka huu, ambako ilifanyika katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya masoko, stendi, minada na maeneo ya wazi. Wananchi walijitokeza kwa wingi kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Kupitia kampeni hiyo wajasiriamali waliofikiwa na elimu hiyo ni 118 na wananchi 2158 na kufanya jumla yao 2,276.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Andreas Whero, aliipongeza TBS kwa kutoa elimu kwa wananchi na alishauri kufanya ukaguzi wa kushtukiza madukani hususani katika bidhaa za ujenzi kama nondo na mabati sambamba na kutumia redio jamii za wilayani ili kufikia wananchi wengi zaidi.

Akizungumza wakati wa kampeni hiyo, Meneja Uhusiano na Masoko TBS, Gladness Kaseka, alisema lengo la shirika hilo ni kutoa elimu kwa umma katika ngazi za wilaya zote.

"Kwa sasa TBS tumeamua kuwafikia wajasiriamali, wafanyabiashara na wananchi katika ngazi za wilaya ili kuwapatia utaratibu unaotakiwa kwa ajili ya kupata alama ya ubora na kusajili majengo ya biashara ya chakula na vipodozi ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza, kwa hiyo elimu hii ya umma ipo katika ngazi ya wilaya na hadi sasa TBS imezifikia wilaya 63," alisema Kaseka

Nao wajasiriamali kutoka vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Malinyi waliipongeza TBS kwa elimu waliyoitoa maana imewafumbua mambo mengi kuhusu umuhimu wa viwango katika bidhaa wanazozizalisha.

Mkaguzi wa TBS, Kaiza Kilango, aliwakumbusha wananchi kutambua kuwa vita ya bidhaa hafifu si ya shirika hilo pekee, bali ni ya Taifa kwa ujumla na hivyo wasisite kutoa taarifa pindi wanapokutana na bidhaa zilizokwisha muda wake au wanapotilia shaka bidhaa yoyote katika soko.

Kaiza aliwafafanulia wananchi umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku vile vile kuwafahamisha fursa ya huduma bure kwa wajasiriamali wadogo na kuwataka wawe mabalozi wa kuhamasisha ubora katika jamii wanazoishi.

Pia aliwataka wafanyabiashara kufuatilia taratibu sahihi za usajili wa bidhaa au majengo ya chakula na vipodozi kwa kutembelea ofisi ya TBS iliyopo karibu au kupiga katika kituo cha huduma kupitia mawasiliano yaliyotolewa.

Kampeni ya kuelimisha umma ni endelevu na itaendelea katika wilaya za mkoa wa Tabora, Mtwara na Lindi.

# MAISHA

SEPTEMBA 10, 2023
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 14


**Ondoa kiriba tumbo**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Je umechagua nyumba imara ya ndoto yako?



Ukurasa 12

**HARUSI**





# Mwanamitindo Mtanzania anayetamba Ulaya

Ukurasa 13

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | |
|---|---|
| KITABU | PENI |
| GOLI | MPIRA |
| FUNGUO | KUFULI |
| BARUA | BAHASHA |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A | | J | I | O | N | I |
| L | | | | B | | M |
| A | | F | A | A | | B |
| S | A | A | | M | T | I |
| I | | T | A | A | | S |
| R | | W | | | | H |
| I | B | A | N | E | | A |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

LIA, GOA, NZI, BUU, ONANA, LUGHA, INAMA, JIONI, ASUBUHI,IMBISHA

## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI





## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU. TUENDELEE NA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU. JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 4 | 2 | 3 | |
| 1 | | 2 | 4 |
| | | | |

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MAMA John alikwenda dukani kumnunulia mwanawe viatu vya shule, aliporudi alimpatia kwa furaha mtoto wake.

Mama: Mwanangu leo nimekuletea zawadi ya viatu.

John: Mama asante nitakwenda kuwaonyesha akina Juma.

Mama: Sawa lakini yule muuza kaniambia kama hujakipenda nirudishe.

John: Mama mtoto huyu sijui kama anasoma kweli!

**SWALI**

Mto Ruvuma unapatikana katika mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Unawajua wanawake mwiba kwa waume zao?

***KARIBU msomaji wangu katika safu yetu hii tuendelee kudadavua yale yanayozisibu familia zetu kila uchao. Wapo wanawake ambao wamekuwa mwiba mkali kwa waume zao kutokana na vituko wanavyowafanyia. Leo tuwasikia wachache.***

“...Pole na kazi. Mimi nina ndoa huu ni mwaka wa saba. Lakini miezi sita iliyopita tuligombana na mke wangu, tena makosa mengi yanatokana na yeye, lakini wazazi wake wanamtetea.

Akakimbilia kwao na wazazi wakampokea. Mimi nikawaambia ndugu zangu wakajaribu kumrudisha japo baba yake alikuwa hataki. Lakini alirudi baada ya kukaa kwao miezi hiyo sita.

Sasa majuzi nikamsikia akizungumza na mtu kwenye simu akimwambia tukutane pale pa siku zote karibu na kibanda cha soda. Fanya booking kabisa jamaa anasafiri. Ni kweli nilikuwa na safari ya kikazi. Hakujua kuwa nilikuwa karibu na nilirekodi mazungumzo yao.

Usiku ilibidi nimuulize huo mpango wake una lengo gani, japokuwa alikana tena kwa machozi! Lakini nilipomfungulia mazungumzo yale kwenye simu na huyo mshikaji wake, akabaki anashangaa. Nikamwambia nimeshajua kuwa anatoka nje ya ndoa, ajitafakari na asubiri hatua nitakazochukua.

Jambo la ajabu ni kwamba akiwa na mipango yake mibaya husababisha tafrani ili tugombane, kisha anatimkia kwao. Kumbe ni ili afanikishe uasi ndani ya ndoa yetu. Kwa kweli ni muda sasa natizama tu sijui nifanyeje!

Mpenzi msomaji, ujumbe huu ulitumwa kupitia simu ya kiganjani hivi karibuni. Hivi majuzi baba mwingine akatuma ujumbe unaokaribia kufanana na huu kuonyesha mchezo huu wa kuigiza unaofanywa na baadhi ya kinamama lakini wanapobanwa na waume zao wanatishia nyau na kukimbilia kwa wazazi wao kwa muda, kisha kurejea.

Ujumbe huu unasema hivi; “Anti, pole na majukumu, naitwa baba J nipo Arusha. Nina mke wa ndoa yenye miaka miwili. Mwenzangu ugomvi ukitokea anafungasha anaondoka anarudi kwao ni Manyara.

Mwaka huu ameshatoroka zaidi ya mara sita na sasa amelianzisha na fununu nilizo nazo anataka kwenda Dodoma. Matatizo ya ndoa yamenitia ganzi mbinu zote nimetumia”. Anamaliza ujumbe wake.

Mpenzi msomaji, sikia vilio vya wanaume kuhusu wake zao watoro ambapo mzozo kidogo wanatimkia kwao, kisha wanarejea kwa waume zao. Je, ni sarakasi gani hii na kwanini unadhani haya yanatokea?

Mpenzi msomaji wangu, bila shaka umewaelewa wanaume hao wanaolia kuhusu wake zao.Yapo mambo mengi yanayochangia hayo kutokea. Ni muhimu kuelewa kwamba mbomoaji mkubwa wa ndoa nyingi ni shetani.

Shetani siku zote huanza kumshambulia mwanamke ili mwanaume wake anayeinukia kiuchumi aanguke. Akivurugwa mwanamke, mwanaume hawezi kupiga hatua za mafanikio. Mwanamke ni msaidizi muhimu sana wa mwanaume.

Shetani akilijua hilo, hutafuta maeneo ya kumshika mwanamke kama kilipuzi. Ataibua tabia ya utoro ambayo imo ndani ya mwanamke husika tokea akiwa mtoto. Lipo jambo linalotokea leo, kumbe lilianzo tangu zamani. Asili zingine ndizo zinazotesa watu wengi. Kama kwenye asili yenu kuna tabia ya ulevi, uzinzi, kuoa na kuacha (roho za mitala yaani wake wengi), wizi, ushirikina, matambiko na kadhalika. Usishangae leo vikakupata wewe.

Watu wengi wamerithi tabia za wazazi wao. Upo msemo wa kiungu kwamba alivyo binti ndivyo alivyo mama yake. Hii ikimaanisha mtu aweza kurithi asili yake.

Wakati mwingine kama baba aliwahi kuoa na kuacha au mama aliwahi kuolewa na kumwacha mumewe katika mazingira fulani, hiyo roho ya mitaala huwaandana pia uzao wao.

Ndiyo maana wazazi wanapoona tabia fulani ikijitokeza kwa watoto wao ukubwani, hawashangai kwani ilianzia kwao. Ndio maana baadhi ya wanawake wenye asili fulani wanapotoroka kwa waume zao, wazazi huwapokea na ajabu zaidi huwatetea kwani wanajua chanzo ni wao!

Hebu msomaji wangu toa maoni au ushauri kuhusu kilio cha jamaa hao wawili waliotoa kuhusu utoro wa wake zao kwenda kwao.

Wiki ijayo nitatoa simulizi fupi mwanamke anavyomnyima raha mumewe kwa tabia ya kutimkia kwao mara kwa mara. Kumbe ni maelekezo ya mama yake mshirikina ambaye ni chanzo cha mimba za binti yake kuharibika kitatanishi.

***Je, una kisa au simulizi ya kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Asilimia 10 mikopo halmashauri imekwamia wapi?

UKITAKA kujua watu wanafikiaje ndoto zao au malengo yao ya kiuchumi, nenda kamuulize ofisa mikopo yeyote nchi hii atakwambia.

Si tu wa benki, si wa Chama cha Ushirika wa Akiba wa Kuweka na Kukopa (SACCOS), nenda hata na benki za jumuiya vijijini (VICOBA) utakutana na msururu wa watu wanaokopa kwa ajili ya kutimiza malengo ya biashara.

Huwezi kufikia malengo makubwa kiuchumi, kufanya biashara kwa ufanisi na kupata tija kama hujawaza kuchukua mkopo. Huo ndio ukweli na ni mtazamo wa kiuchumi.

Lakini kama mnavyojua, wengi wetu hatukopesheki katika benki na taasisi za kifedha kwa sababu ya vigezo vya kukopesheka.

Kubwa zaidi, makundi haya yanaogopa au kukimbia riba kubwa inayotozwa kwenye mikopo ya taasisi kubwa za fedha nchini.

Ndiyo maana sasa hivi ukisikiliza au kufuatilia vyombo vya habari kuhusu taarifa za mikopo, habari kubwa ni mtu amejiua kwa sababu ya kudaiwa marejesho ya mkopo na kikundi au vikundi vinavyojiita 'kausha damu'

Tusiruhusu watu wetu kupoteza maisha kwa kujitoa uhai ili kuepuka fedheha au kufilisiwa na kikundi cha watu wanaotoka hizo zinazoitwa taasisi za kausha damu.

Kwa nini waraka huu nauandika kwa sasa? Jibu ni kwamba serikali ilisitisha mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na kila halmashauri, ikieleza nia yake ya kujipanga kuweka mfumo mpya wa utoaji wa mikopo hiyo.

Aprili 13, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza uamuzi wa serikali kusitisha mikopo hiyo ya asilimia 10.

Waziri Mkuu Majaliwa, ndiye aliyetoa amri hiyo, akizielekeza halmashauri zote nchini, kusitisha utoaji wa fedha za mikopo kwa makundi maalum ya vijana, wanawake na wenye ulemavu kuanzia Aprili hadi Juni, 2023.

Wanaokumbuka watanisahihisha kama nimepotoka. Lakini alitangaza uamuzi huo wa serikali, alipokuwa akihitimisha hoja zilizotolewa na wabunge, wakati wakijadili mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/24.

Uamuzi wake kimsingi, ulichagizwa na hoja za wabunge zilizoonyesha kuna sehemu inavuja katika muktadha mzima wa utoaji wa mikopo hiyo.

Wengi walipiga kelele kuhusu kiasi kidogo cha fedha za mikopo zitokanazo na asilimia 10 ya makusanyo ya halmashauri kinachotolewa kwa makundi maalum ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kutokidhi matakwa ya kuyainua makundi hayo kwa kufanya shughuli za uzalishaji au biashara.

Katika hoja hizo ilielezwa kuwa kumekuwa na changamoto kwenye baadhi ya halmashauri kutoa fedha hizo kwa watumishi wa halmashauri au wakati mwingine vikundi hewa, badala ya walengwa na kusababisha fedha za mikopo hiyo kutorejeshwa.

Pengine, wabunge walisukumwa na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa Machi 29, mwaka huu, wakati akipokea taarifa ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, kwa mwaka 2021/2022.

Wakati anapokea ripoti hiyo ya CAG, Rais Samia aliagiza kuangaliwa upya kwa utaratibu wa utoaji wa mikopo ikiwemo kuangalia namna ya kutumia mabenki kupitishia mikopo hiyo.

Bila shaka, Rais Samia alirejea na yeye kuikumbusha Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba wakati inaandaa miongozo na taratibu za kutoa mikopo hiyo, na waraibu wa dawa za kulevya wajumuishwe kwenye mpango huo ili kuwasukuma wajishughulishe na ujasiriamali utakaowainua kiuchumi.

Si hao tu waraibu wafikiriwe, kuna kundi la kinababa nao hawamo. Wanaojua Biblia, kitabu cha Waefeso 5:23-32 kimeandika kwa maana mume ni kichwa cha mke kama vile Kristo alivyo kichwa cha kanisa, ambalo ni mwili wake, naye mwenyewe ni Mwokozi wa kanisa. Basi, kama vile kanisa linavyomtii Kristo, vivyo hivyo na wake pia wanapaswa kuwatii waume zao kwa kila jambo.

Kutokana na hayo maandiko ya Biblia, kati yetu nani ambaye hajasikia baadhi ya wanaume wanalia hivi sasa kwamba mke wake kainuka kiuchumi, yeye sasa ndio ananyanyasika?

Eti baada ya kuwa na kipato kumzidi mumewe, hivi sasa baadhi ya wanawake wamesahau iliandikwa mume ni kichwa cha nyumba? Kiburi mtindo mmoja na wengine wanawachapa makonde wakiinua mdomo kusema madhila anayokutana nayo huko kwenye ndoa.

Ikiwapendeza watunga sera, Ofisi ya Waziri Mkuu, kabla hamjairejesha mikopo hiyo waingizeni na kinababa ili mizani ikae sawa.

Na hizi kanuni za sasa za utoaji wa mikopo na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2019, na tangazo la serikali, namba 286 la mwaka 2019, lifanyieni marejeo ya kisheria.

Hebu tuutendee haki ule mpango wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano 2016/2021 na sheria ya fedha ya serikali za mitaa, sura ya 290, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2018, ambavyo viliasisi mikopo hii.

Hii ndiyo sheria na mpango wa Maendeleo wa Taifa, uliloweka masharti kwa halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Tunataka pia serikali ifanye marekebisho ya kanuni ya sita ya sifa za kupata mkopo huo; ambayo kimsingi haijawataja akina baba (wanaume) kwamba nao wanapaswa kuwa wanufaika.

Kila mtu ana nafasi ya kung'ara kwenye eneo lake. Hakuna nyota inayozuia nyota nyingine kuonekana angani, ila usisahau kuwa kila nyota huwa inatofautiana nguvu ya kung'ara kwake.

Badala ya kuhangaika kuzuia nyota nyingine kung'ara, weka bidii kuongeza mng'ro kwenye nyota ya kwako.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490***

# HARUSI



Nguo za Kiafrika ni moja ya pambo zuri katika sherehe za harusi, pichani ni aina ya mavazi yanayovaliwa wakati wa kufunga ndoa.

# MITINDO







ZARA BEDAL

## Mwanamitindo Mtanzania anayetamba Ulaya

MWANAMITINDO Mtanzania Zuhura Bedal Said, maarufu kama Zara anazidi kupata umaarufu katika nchi za Ulaya na kufanikiwa kuyateka makampuni mbalimbali yanayojihusisha na mavazi.

Ikiwa ni mara yako ya kwanza kufika katika nchi za Ujerumani na Italia, utakutana na mabango ya kibiashara yenye picha ya mrembo huyo yakipamba maeneo tofauti.

Akizungumza na Nipashe, Zara amesema kipaji chake cha uanamitindo kilianza tangu akiwa mtoto, anafurahia kuona ndoto yake hiyo imeanza kutimia.

Amesema umaarufu anaopata kupitia tasnia hiyo, hautasababisha yeye kubweteka, bali atafanya kazi kwa bidii zaidi ili kufikia malengo yake.

Zara alizaliwa Juni 26, katika eneo la Mkunazini, na kisha kupata elimu ya msingi na sekondari katika shule ya Hamamni iliyoko Zanzibar.

Ameeleza wakati fulani alitamani kufanya kazi katika usafiri wa anga, lakini hakufanikiwa kupata ajira na badala yake aliamua kujikita zaidi katika mitindo.

"Huku kwenye mitindo nimepata mafanikio na ndiko moyo wangu unapenda zaidi," amesema.

Ameeleza katika tasnia hiyo hakuna njia ya mkato inayoweza kupata mafanikio, bali ni lazima ujitume na kujitambua wewe ni nani na unataka kufanya nini.

Amesema kwamba kutokana na moyo wake wa kazi, alianza kupata kazi kidogo ya matangazo na sasa anaaminiwa kwa kupewa mikataba ya kutangaza bidhaa katika kampuni kubwa.

Ameeleza kwamba anataka kuona jina lake linazidi kuwa kubwa ili hata vijana wanaotaka kuingia katika tasnia hiyo kuwa mfano mzuri kwao.

"Watu wanaotamani kuwa na ndoto za kuingia katika ulimwengu wa wanamitindo wanataka kuwa kama mimi, wanaitizama kila hatua ninayochukua, ni vizuri nikawaonyesha kila kitu kizuri kuliko kuwakatisha tamaa," amesema.

Zara kwa sasa anafanya kazi nchini Ujerumani, ameshiriki katika kutangaza chapa maarufu duniani kama Dolce & Gabbana, Stella McCartney, Adidas, Karl Lagerfeld, Tiger of Sweden, Level shoes ya Dubai, na Landeros iliyoko jijini New York.

Umahiri wake wa ajabu katika mitindo, pia amepamba majarida maarufu ikiwamo Vogue, Bazaar, Marie Claire, Elle, Maxmara, Meno, Zahrat Al Khaleej na Nawa3em.

UREMBO



# Ondoa kiriba tumbo

MIAKA ya zamani, tumbo kubwa lilihusishwa na utajiri au uwapo wa mafanikio kwenye maisha.

Mambo yamebadilika, tumbo kubwa au kiriba tumbo limekuwa tatizo kubwa hususani kwa wanawake ambao hupoteza urembo wao.

Tumbo kubwa pia linaondoa utanashati kwa wanaume, nguo kubana tumbo na kukosa kipimo chako.

Kwa kuwa baadhi ya aina za mafuta zinazojikusanya tumboni huwa siyo nzuri, tumbo la aina hii linaweza kuwa chanzo cha magonjwa sugu.

**Hatua za kupunguza tumbo**

**Chai ya rangi**

Chai ya rangi huwa na kemikali muhimu kwa kuunguza mafuta ya tumbo, huitwa epigallocatechin gallate.

Kemikali hizi kwa miaka mingi zimekuwa zinatumika katika kutengeneza vyakula na vinywaji kwa ajili ya watu wanaotaka kupunguza tumbo.

Ufanisi wake huongezeka zaidi kwa watu wanaofanya mazoezi, pia ikichanganywa na limao au ndimu.

**'Apple cider vinegar'**

Umewahi kwenda kwenye maduka makubwa ukakutana na chupa imeandikwa kwa majina hayo?

Hiyo chupa ni chaguo sahihi kwa watu wenye tumbo kubwa.

Huwa na kemikali za acetic acid ambazo tafiti nyingi zinathibitisha uwezo wake wa kuunguza mafuta ya tumbo.

Kiasi cha vijiko viwili kwa siku vilivyo changanywa kwenye maji vinatosha kabisa kuleta majibu chanya.

**Usingizi**

Kulala muda mrefu ni afya, hakikisha unalala kwa saa 9 hadi 12 kwa siku ili kupunguza tumbo.

Usingizi ni dawa njema pia kwa afya ya mwili na akili, ukifanya hivyo utapunguza kitambi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya tango

WATU wengi wamezoea kutumia tunda la tango kama kiburudisho na kiungo cha mboga hususani kwenye utayarishaji wa kachumbari na saladi.

Baadhi wanatumia kama pambo la kunogesha sahani mezani na kuongeza hamu ya kula.

Lakini pia tango huweza kutengeneza juisi tamu yenye faida nyingi mwilini.

Hutumiwa kama moja ya kinywaji cha kusaidia kupunguza uzito na kitambi.

**Maandalizi**

Osha matango kwa maji safi na uyakate kwa vipande vidogo vitakavyoweza kusagika. Fanya hivyo pia kwa tangawizi.

Ukimaliza kamua limao na uchuje tayari kwa ajli ya kuchanganya na juisi yako ikishakuwa tayari

andaa blenda na uweke vipande vyote kwenye blenda na vikombe viwili vya maji, kisha saga.

Ikishasagika vizuri ongeza mdalasini na usage tena, ikimalizika chuja na uweke kwenye glasi. Ongeza vijiko viwili vya maji ya ndimu, vijiko viwili vya sukari pamoja na vipande vya barafu.

Juisi yako ipo tayari kunywa, unaweza kuweka kwenye friji kwa ajili ya matumizi ya baadae.



MAISHA NI NYUMBA
Na Restuta James

## Unajua viungo ni pambo?

HILIKI, mdalasini, tangawizi iliyokaushwa, mchaichai, karafuu, karanga na mahindi ya bisi ni pambo zuri, kama likipangiliwa vyema.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Esther Donald, anasema ili kutumia pambo la aina hiyo, unapaswa kuwa na jagi maalumu la kioo au linaloangaza.

Anasema unachopaswa kufanya ni kuweka tangawizi iliyokaushwa kiasi, karafuu na hiliki.

"Inategemea na ukubwa wa chombo chako cha kupambia, unaweza kuweka nusu kikombe cha chai cha kila kiungo. Kila kimoja kinapaswa kuonekana kwa hivyo usivikoroge," anasema.

Esther anasema pambo la viungo linaweza kuwekwa kwenye stendi eneo la chakula (dining) au sebuleni ambako mchanganyiko unaweza kuwa wa karanga na korosho.

Hata hivyo, anashauri kwamba pambo la viungo linaweza kuboreshwa kwa kuwekewa jagi lingine lenye maua kama inavyoonekana pichani.

**Tuwasiliane kupitia restutajames@gmail.com au 0753333330**





# Je umechagua nyumba imara ya ndoto yako?

UIMARA wa nyumba ni kuhimili mambo mengi ikiwamo changamoto zinazojitokeza nyakati za mvua, upepo mkali na uzito wowote unaoipiga.

Peter Akoye, anayejishughulisha na masuala ya ujenzi wa nyumba, anasema uimara na uzuri wa nyumba unategemea vitu vingi.

Kwamba, kwa nyumba za kawaida, uimara wake huanzia kwenye ujenzi wa msingi, kuta, paa, nguzo, milango, madirisha na dari ambayo yote haya yanapaswa kuzingatiwa wakati wa ujenzi wake.

"Nyumba imara na mwonekano mzuri ni alama kwa eneo husika, huongeza thamani ya jengo, mandhari ya jengo iliyowekwa katika uzuri, pia huleta hisia na utulivu, furaha na uchangamfu kwenye familia na mtaa.

"Ni muhimu jengo liwe imara na uzuri unaoendana na matumizi yake, kama ni kwa ajili ya biashara, basi liwe lenye mvuto unaovutia hata wateja, kama ni kwa ajili ya kuishi familia, basi ichangie kuleta amani na furaha nyumbani," anasema.

Anashauri kwamba ni vyema nyumba ikafanyiwa usanifu mzuri na bora kuanzia jengo lenywe, mazingira ya ndani, mandhari ya nje ili yabebe maana fulani na kwamba ni muhimu kuwa makini na maana hiyo unayomwambia mtu kupitia nyumba yako.

"Rangi, mpangilio, mpishano, kimo, ukubwa, umbile la nyumba yako huathiri hisia za mtumiaji. Pia niwakumbushe kwamba rangi nyeupe kwenye nyumba huleta hisia za usafi, utaratibu na amani.

"Kijani huleta hisia za utulivu, uasili. Nyekundu huleta hisia za kusisimua, shauku, changamfu. Rangi ya waridi huleta hisia ya furaha na ya bluu huleta hisia za uasilia na utulivu pia, kwa hiyo ni muhimu kufanya chaguo sahihi unapopanga au unapokamilisha ujenzi wa nyumba ya ndoto yako," anasisitiza.






Anashauri kwamba jambo la msingi ni kujenga nyumba unayohitaji, itakayokidhi mahitaji ya sasa na baadae, yenye usalama na uimara, iliyo katika uzuri wake na kuepuka kujenga usiyoihitaji.

Kufahamu aina ya nyumba inayokufaa kujenga ni miongoni mwa jambo linalosisitizwa na mtaalam huyu kwa kuwa ndiye mahali muhimu ambapo kila mtu anapatia faraja na kupata muda wa kupumzika baada ya shughuli nyingi za kujitafutia kipato.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
VIPI SHOSTI MBONA UMEGANDA KAMA UMESIKIA TAARIFA MUMEO KAOA SHOGA YAKO!
NASHANGAA UGOKO MKAVU LAKINI BADO NA KIMINI...!
JUKWAANI
SIASA 'BOVU'
MDOMO.... UNATAKA KUNAMBIA SHUGHULI YAKO ILIISHIA KWENYE KUNISAIDIA KUROPOKA TU!...
ETI BABY NASIKIA UNASEMA MIYE MPENZIYO KIMEO?
NAANZAJE KWA MFANO JAPO UPO UPO HUELEWEKI!
HIVI KUACHWA KUMWAGWA, KUTOSWA AU KUFURUMUSHWA NENO LIPI LINAUMA?
NAKUSINDIKIZA KWA MKEO JARIBU KUJIKAZA ASIGUNDUE KAMA TUMELEWA... 'UTAFANYAJE?
NITAKUMBATIA NGUZO YA BARAZA ILI NISIYUMBE
EMBU JAMANI TUWE WASTAARABU SIO KILA NENO LINAFAA KUJADILI HUMU!
WEWE ACHA UNOKO WAKO! NDANI YA DALADALA NDIO ENEO LA MAZOEZI YA 'UBUNGE' TUNACHAMBUA NA KUJENGA HOJA BILA NDUGU SPIKA...
NA MIFOLENI HII UNATAKA TUNUKE MIDOMO?
WE BHANA KAA KIMYA NDIO NYIE WAROPOKAJI WENYEWE
MPIGIENI MAKOFI.... KUNA WENGINE HUMU WANA'STRESS ZA KUKUTANA NA WAKE ZAO MAJUMBANI 'WESHENUNIWA'
NA MIDUME INAYONUNA JE?
MBONA NNA WASIWASI KAMA NAKOGA NJE?
NGOJA NIENDE BAR NIKAMEZE DAWA YA KUMBUKUMBU
BOSI ULIMI WAKO HAUNA BREKI!
KANTAFUTIE 'MAKENIKA' AJE NA SPANA ZAKE
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KILA UKIONA MANYOYA KALIWA....

## AU mwanachama wa kudumu G20

**NEW DELHI,** India

WAZIRI Mkuu wa India Narendra Modi, ameutangaza Umoja wa Afrika (AU) kuwa mwanachama wa kudumu wa kundi la mataifa tajiri na yale yanayoinukia kiuchumi la G20.

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa mkutano huo, Modi, aliualika Umoja wa Afrika unaowakilishwa na mwenyekiti wake Azali Assoumani, kuchukuwa nafasi yake katika kundi hilo kama mwanachama wa kudumu.

Modi aliongeza kuwa hatua hiyo italiimarisha kundi hilo na nchi zenye viwango vya chini vya kiuchumi na maendeleo.

Umoja wa Afrika wenye mataifa wanachama 55, sasa una hadhi sawa na Umoja wa Ulaya, kundi la pekee la kikanda lenye uanachama wa kudumu katika G20.

Hadhi yake ya awali katika G20, ilikuwa shirika la kimataifa lililoalikwa. **DW**

## Putin aishika mkono Korea Kaskazini

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia Vladmir Putin ametoa wito wa kuimarisha ushirikiano katika nyanja zote na Korea ya Kaskazini.

Kauli ya kiongozi huyo ilitolewa wakati akimpongeza Rais wa Korea Kaskazini Kim Jong Un kwa kuadhimisha miaka 75 tangu kuanzishwa kwa taifa lake.

Maadhimisho hayo yaliyoanza Ijumaa usiku yamefanyika wakati kukiwa na matarajio kuwa Kim Jong Un atasafiri kwenda Russia hivi karibuni kukutana na Rais Putin. Maadhimisho hayo yamehudhuriwa na ujumbe kutoka China ukiongozwa na Naibu Waziri Mkuu, Liu Guozhong wakati Russia ikiwa imetuma kikundi cha dansi na wimbo wa kijeshi.

Vyombo vya habari vya Korea Kusini vilisema kukosekana kwa wawakilishi wa serikali ya Russia kwenye mkutano huo ni ishara ya maandalizi ya mkutano kati ya viongozi hao ambao huenda ukafanyika wiki ijayo. Mkutano huo huenda ukajikita katika makubaliano ya kuuza silaha za Korea Kaskazini kwa Russia ili kuongeza akiba. **DW**

# Buthelezi afariki dunia



**NATAL,** Afrika Kusini

KIONGOZI wa kabila la Wazulu nchini Afrika Kusini, Mangosuthu Buthelezi, ambaye pia ni waziri mkuu wa kitamaduni wa taifa la Zulu, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 95.

Buthelezi,ambaye amekuwa mmoja wa viongozi wakuu wa kisiasa nchini humo katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, aliongoza kabila la Wazulu chini ya utawala wa ubaguzi wa rangi.

Akiwa mjumbe wa baraza la mawaziri la Nelson Mandela, aliwahi kuwa waziri wa mambo ya ndani kwa muongo mmoja.

Rais Cyril Ramaphosa aliongoza ibada maalum, akimtaja Chifu Buthelezi kama kiongozi wa kutisha.

"Mfalme Mangosuthu Buthelezi amekuwa kiongozi bora katika maisha ya kisiasa na kitamaduni ya taifa letu, ikiwa ni pamoja na mtiririko wa mapambano yetu ya ukombozi, kipindi cha mpito ambacho kilinda uhuru wetu mwaka 1994 na utawala wetu wa kidemokrasia." alisema Ramaphosa.

Chifu Buthelezi alikuwa mwanzilishi wa chama cha Inkatha Freedom Party, ambacho kiliendesha vuguvugu la kisiasa na kitamaduni la Wazulu.

Alishirikiana na chama cha African National Congress (ANC) katika mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi na kufanya kampeni ya kuachiliwa kwa Nelson Mandela.

Lakini akawa mkosoaji katika miaka ya 1980, akishutumu chama hicho kwa kuunga mkono upinzani wa kutumia silaha kwa serikali kibaguzi na aliunga mkono wake kwa vikwazo vya kimataifa. **BBC**



Mwanamke akipita katika jengo lililoporomoka huko Marrakesh, baada ya tetemeko kubwa la ardhi kutokea usiku wa Ijumaa. **PICHA: REUTERS**

# Tetemeko la ardhi laua 820 Morocco

**RABBAT,** Morocco

IDADI ya watu waliokufa katika tetemeko la ardhi nchini Morocco inazidi kupanda, mpaka jana jioni watu 820 wamethibitishwa kupoteza maisha katika tukio hilo.

Televisheni ya taifa ya Morocco ilisema ikinukuu takwimu za wizara ya mambo ya ndani na kueleza inatarajiwa idadi kuongezeka.

Wizara hiyo ilisema takriban watu 672 walijeruhiwa katika mkasa huo, wakiwamo 205 ambao wako katika hali mbaya.

Morocco iliwahi kushuhudia matetemeko makubwa ya ardhi hapo awali, ikiwamo mwaka wa 2004, tetemeko la ardhi lilipiga eneo la al-Hoceima kaskazini-mashariki mwa Morocco na kuua watu 628. Mwaka 1960, tetemeko la ardhi la Agadir liliua watu 12,000.

Kitovu cha tetemeko la ardhi lililotokea jana usiku kilikuwa katika milima ya Atlas. Kuna vijiji vingi vya mbali ambavyo vimekumbwa havijafikiwa mpaka jana.

Inaweza kuchukua siku nyingi kabla ya kujua ukubwa wa janga hilo.

Ripoti zinasema changamoto kubwa ni kufikia watu katika vijiji vya mbali katika milima ya Atlas ambavyo viliathiriwa vibaya na tetemeko la ardhi.

Huenda ikachukua muda kabla ya waokoaji kufika vijiji hivyo ambavyo vina majengo mengi ya zamani.

Tetemeko hilo lilifika hadi katika visiwa vya Canary karibu na pwani ya Morocco na Algeria.

Kumeshuhudiwa watu walipata mshtuko wakikimbia nyumba zao na kwenda mitaa ya Marrakesh kujinusuru.

Tetemeko hilo lenye ukubwa kipimo cha 6.8 limekumba eneo lote la kati la Morocco.

Utafiti wa jiolojia uliofanywa Marekani ulieleza kitovu cha tetemeko hilo kilikuwa katika milima ya juu ya Atlas, kilomita 71 kusini-magharibi mwa Marrakesh.

Tetemeko hilo lilitokea saa tano na dakika kumi na moja usiku wakati watu wakiwa majumbani mwao.

Kulikuwa na mitetemeko yenye ukubwa wa 4.9, iliyofuata dakika 19 baadaye.

"Kulingana na ripoti ya muda, tetemeko la ardhi liliua watu 296 katika majimbo na manispaa ya al-Haous, Marrakesh, Ouarzazate, Azilal, Chichaoua na Taroudant," ilisema taarifa hiyo ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Baadhi ya majengo katika mji wa zamani wa Marrakesh yameporomoka, mkazi mmoja aliambia shirika la habari la Reuters.

Klipu kadhaa kwenye mtandao wa X zinaonyesha majengo yakianguka, lakini BBC haijabainisha ni wapi. **BBC**

MAKALA

# UTEUZI UZINGATIE TAALUMA HUSIKA



Na Magabilo Masambu

TANZANIA kama nchi nyiginezo duniani ina mfumo wa kuwapata viongozi. Moja wanapatikana kwa kuchaguliwa na wananchi au kuteuliwa. Wanapochaguliwa baadaye wako wanaoteuliwa katika nafasi mbalimbali. Ukichaguliwa kuwa mbunge unaweza kuteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri.

Kuna viongozi wanaochaguliwa huku wakiwa na taaluma zao. Mfano mtu anachaguliwa na wananchi kuwa mbunge lakini yeye kitaaluma ni mhandisi wa majengo au umeme au kilimo. Si wote wanaochaguliwa ni wataalam kwa sababu Katiba ya nchi yetu inasema ili kuwa mbunge, kwa mfano, unatakiwa kuwa na umri kuanzia miaka 21 na ujue kusoma na kuandika. Kwa maana hiyo, wako wabunge ambao ni darasa la saba tu.

Kwa mujibu wa Katiba, ili kuwa waziri katika wizara yoyote sharti uwe mbunge ama kwa kuchaguliwa au kwa kuteuliwa. Kwa maana nyingine, kila waziri ni mbunge lakini si kila mbunge ni waziri. Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakijiuliza hivi sifa ya kuwa waziri ni ipi? Vigezo gani vinatumika kumteua mbunge kuwa waziri? Je, ni taaluma, uzoefu, umri au ni nini hasa?

Tumeshuhudia mara kadhaa, baadhi ya watu wakiteuliwa katika wizara ambazo si taaluma zao. Ukiuliza utaambiwa kuwa pale wizarani kuna mtu anaitwa katibu mkuu na kwamba huyo ndiye anatakiwa kuwa mtaalamu katika wizara. Jambo hili limekuwa likisumbua kidogo.

Kwa mtazamo wangu, watu wateuliwe kutokana na taaluma zao ili tunapowahukumu kutokana na utendaji wao, wasipate cha kujitetea. Sababu zangu ni kwamba, kwanza, ni kutafuta ufasini katika nafasi mbalimbali si tu kwenye nafasi za uwaziri lakini hata kwingine. Kwa kweli kumteua mwalimu wa Kiswahili kusimamia maabara ya Kemia ni kumwonea japo hataweza kukataa kwa sababu inawezekana ikawa ni nafasi yenye malipo mazuri.

Mabadiliko ya mara kwa mara ambayo yamekuwa yakifanywa serikalini, maelezo yake ni kwamba ni katika kuboresha utendaji, lakini tunaweza kujikuta tukiwalaumu watu bure kuonekana hawajui kazi, lakini kumbe wanapewa vitengo vyenye taaluma tofauti na walizozisomea. Mfano, kumchukua mwandishi wa habari kusimamia sekta ya ujenzi au daktari wa binadamu kusimamia sekta ya nishati, inaweza kuleta shida katika usimamizi kwa sababu ni rahisi kudanganywa anaweza kuelezwa na vitu ambavyo havipo na akakubali kwa sababu havijui.

Wakati tunasoma sekondari miaka hiyo, ilikuwa kawaida kabisa mwanafunzi kwenda nyumbani na kumdanganya mzazi kwamba wameagizwa assemble (eneo la kukusanyikia wanafunzi) na kwamba hiyo 'asembo' inauzwa! Kwa hiyo mwanafunzi anataka pesa kutoka kwa mzazi akainunue. Hii ni kwa sababu wazazi wengi hawakuwa na elimu ya sekondari. Leo ni vigumu sana kumdanganya mzazi kwa sababu wengi wamesoma wanajua 'asembo' maana yake ni nini. Ndivyo inavyoweza kutokea kwa kiongozi asiye na uelewa wa sekta fulani mwisho wa siku ataonekana hafanyi kazi na kulaumiwa.

Hoja inaweza kuibuka kwamba mbona Rais wa nchi anweza kuongoza na hana taaluma zote hizo? Ni sawa, lakini bado mtaalam wa fani isiyokuwa yake wakitaka kumdanganya watamdanganya na hatajua kama amedanganywa. Kinachowafanya wengi waogope ni viapo walivyokula wakati wa uteuzi lakini tunaona hata Katiba bado inatamka kwamba mtu kuwa Rais wa Tanzania anatakiwa angalau kuwa na shahada ya kwanza, maana yake umuhimu wa taaluma unatambulika bado.

Ni kweli kwamba si jambo baya kumteua mtu kwenye sekta isiyo taaluma yake, lakini ingekuwa vizuri sana kama mwenye taaluma ya yake akasimamia sekta inayomhusu. Inawezekana mazoea haya yalitokana na awali wataalamu walipokuwa wachache, hivyo kutopata kila mtaalamu na sekta yake kwa sababu waliosoma wakati huo walikuwa wachache, hivyo kulazimika kumchukua yeyote awe popote. Lakini sasa nadhani hakuna tena haja hiyo kwa sababu wasomi na wataalamu wamejaa kila kona ya nchi.

Athari zinatokana na uteuzi wa mara kwa mara, pengine kutokana na utendaji usioridhisha ambao naona sababu mojawapo ni hiyo ya taaluma. Moja, viongozi wanaohamishwa mara kwa mara inafika wakati wanashindwa kujiamini na matokea yake wanaharibu kila wanakokwenda. Athari nyingine ni kwa wananchi wanaohudumiwa. Wananchi kila wakati wanakutana na sura ngeni ofisini jambo linalowafanya wakati wote wawe watu wa kujieleza upya kwa viongozi wageni.

Mfano, una tatizo la ardhi umekwenda ofisini wiki hii umekutana na mkurugenzi Fulani, mmezungumza mkaweka mambo sawa, wiki ijayo unakwenda unakutana na sura mpya unaanza tena kujieleza. Wengine wanasema mimi ni mgeni ndiyo kwanza nimefika nitashughulikia, ndiyo imetoka hivyo.

Nadhani uteuzi kwenye maeneo yanayohitaji utaalamu, wateuliwe wenye taaluma hizo. Mbona mahakamani hatupeleki mwalimu maana yake atashindwa kutafsiri sheria, japo wanasheria hao wamefundishwa na mwalimu huyo.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Wakwe wanapochoka kulisha binti yao na mumewe*



Na Adam Fungamwango

SIKU hizi wamezuka vijana ambao wanachukuliwa na baadhi ya wanawake wenye umri mkubwa na kuwekwa ndani. Nikisema kuwekwa ndani sina maana na kufungwa jela bali wanahudumiwa kwa kila kitu kuanzia kula, mavazi, malazi na hata kupewa magari.

Imefika wakati siku hizi mambo haya yanafanywa na baadhi ya wanawake ambao hawana hata umri mkubwa. Mradi tu na yeye akiwa na kazi yake nzuri, pesa na maisha bora, anamtafuta kijana mmoja na kummiliki. Wenyewe wanawaita 'vibenteni.'

Visa hivi vimesimuliwa zaidi kwenye wimbo wa bendi ya TP OK Jazz, utunzi wake Luambo Luanzo Makiadi Franco unaoitwa 'Mario.'

Ni wimbo wa katikati ya miaka ya 1980. Miaka michache kabla ya kifo chake mwaka 1989, Franco aliachia albam moja matata iitwayo 'Mario,' iliyobeba jina la wimbo huo inayomzungumzia kijana mmoja mwenye tabia ya kupenda kulelewa na wanawake wenye pesa.

Wimbo huo ulinyanyasa dunia nzima ndiyo maana hadi leo hii, pamoja na kwamba una miaka mingi sana tangu utoke, jina la Mario bado linatumika na vijana wa vizazi vya sasa.

Kijana yeyote ambaye hapendi kazi, badala yake anajiegemeza kwa kinamama wenye mapesa na kulelewa anaitwa Mario, ingawa hivi karibuni limeongezewa msamiati mwingine usio rasmi, 'kibenteni.'

Inawezekana ukadhani kuwa tabia hiyo imezuka kwa vijana wa vizazi vya sasa. Hapana. Tabia hii ilianza zamani sana, ila siku hizi kuna aina tu au staili ya vijana hao wavivu, wasiotaka kufanya kazi, kujituma, wanaopenda maisha ya juu na anasa kwa njia ya mkato.

Pamoja na mambo mengi yasiofaa kwenye jamii ukiwemo wizi, ujambazi, utapeli, lakini pia, wanapenda kujiegemeza kwa aina hiyo ya wanawake wanaowachukua na kuwaweka ndani na kuwa vimada.

Zamani hawakuwepo sana vijana au watu wa aina hii kwa sababu wanawake wengi hawakuwa sawa kichumi, badala yake walitegemea wanaume ili kuishi, tofauti na sasa ambapo wamesoma, wanajituma, na wamekuwa wafanyabiashara wakubwa hivyo wengi wao kuwa na uwezo mkubwa kiuchumi.

Vijana hawa zamani walikuwa wanajiegemeza kwa wanawake kwa kuishi kwa wakwe zao.

Kijana anaoa mwanamke kumbe hana kitu, badala yake anakwenda kukaa ukweni.

Hii ndiyo ilikuwa staili ya 'Umario' wa zamani kwenda kuishi kwa baba mkwe kwa matumaini au ahadi kuwa wanakaa kwa muda mpaka hapo hali yao ya maisha itakapokuwa nzuri.

Hata hivyo, wengi wao wanaishia kufukuzwa kwa kashfa na aibu. Kwa sababu lengo halikuwa kukaa kwa muda ili wajitafute, bali ilikuwa ni kukaa moja kwa moja kutokana na tabia tu za uvivu na kushindwa kufanya kazi.

Kwa vijana wa sasa naona hawana tabia na kukaa kwa wakwe zao kama wa zamani, ila wanapenda kulelewa.

Na wale wa zamani hao walikuwa hawaoni hata aibu kuishi kwenye nyumba ya baba mkwe wake, yeye na mkewe, kiasi kwamba anakosa uhuru wa kutosha. Hawezi kujimwambafai kama baba, kwa sababu anakuwa kama ni mmoja tu wa watoto kwenye familia hadi hapo atakapochokwa.

**Ni wimbo wa katikati ya miaka ya 1980. Miaka michache kabla ya kifo chake mwaka 1989, Franco aliachia albam moja matata iitwayo 'Mario,' iliyobeba jina la wimbo huo inayomzungumzia kijana mmoja mwenye tabia ya kupenda kulelewa na wanawake wenye pesa.**

Kuna kijana mmoja yalimpata kwa kukaa kwa wakweze, na kisa hiki kikasimuliwa na bendi ya Juwata Jazz. Ulikuwa utunzi wa mwanamuziki Said Mabera, wimbo unaitwa 'Radhi ya Wazazi.' Wimbo huo unaimbwa hivi;-

"Ndugu yangu nakumbuka ulipokuwa mtoto wa miaka 18, ulikosa radhi ya wazazi wako, mimi nilikuchukua ili tukae wote pamoja, kazi nilikutafutia na nikakuoza mke, leo mashangaa nyumba niliyokuba kuishi na mkeo, umeikimbia umehakia ukweni.

"Umekubali kuuza nyumba na kununua kiwanja, kweli radhi ya wazazi wako umekupata.

Wakwe zako umenifuata, kunilalamikia unawabana humu ndani.

Kati ya wewe na mkeo nani kaolewa? Wamechoka kulisha mke wa mume.

Akifukuzaye, hakwambii toka, utaona mambo yanabadilika."

Huyu jamaa pamoja na kufanyiwa yote na ndugu yake, akauza kila kitu na kukimbilia kuishi ukweni. Sasa Wakwe wamemchoka, hamwambii mwenyewe, wanakwenda kunung'unika kwa ndugu yao. Wamechoka kulisha mke na mume.


**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibuni eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

# Kafie Kwenu-10

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Catty alimtazama kwa makini James, halafu akatikisa kichwa kuonyesha kumuonea huruma na pia hawezi kupata kitu chochote anachohitaji kutoka kwa ndugu yake Carry.

"Nipe ushauri basi Catty, nifanyeje mwenzako?"

"Sijui kama unaweza kuukubali ushauri wangu kwa sababu ni mgumu sana."

"Mgumu!?" Akauliza na kushangaa kwa wakati mmoja.

"Mgumu kama utashupaza shingo, lakini kama ukiufuata ni rahisi sana."

James akawa na hamu na haraka ya kutaka kuusikia ushauri huo ambao anataka kupewa na Catty, ndugu yake Carry.

"Usihangaike na mtu asiyekupenda siku zote. Carry ni sistaduu, anapenda mambo makubwa, anapenda maisha ya juu na vitu vya gharama, hawezi kuwa na mwanaume kama wewe, anataka wa hadhi ya juu wenye pesa, mali, vyeo, hadhi. Na siyo yeye tu, wasichana wengi wa kisasa ndivyo walivyo."

James alinyamaza kimya. Maneno yalikuwa yanamuingia na kuyaelewa, lakini bado akili yake ilimtuma kukataa.

"Tafuta wa saizi yako. Usipende kudhalilishwa na kila mwanamke unayekutana naye barabarani. Kuna wengine watakukataa kistaarabu lakini wengine watakudhalilisha kama anavyokufanya dada yangu." Akaongezea nyundo nyingine.

"Ukisema wa saizi yangu ni yupi na nani?"

"Hivi Carry ni mwanamke wa kwanza kukudhalilisha?"

"Hapana, tena hilo mimi nishesHazoea, ila kwa Carry naona kama baadaye anaweza kunielewa vile!"

Catty akaangua kicheko, halafu akamwambia, "hawezi kukuelewa na hatokuelewa milele, tafuta wa hali ya chini na anayekupenda kwa dhati. Ambaye anafuata upendo wako, si maslahi, maisha au fedha."

"Hata wa hali ya chini wengine wananinyanyapaa ujue!"

"Sawa, ila endelea kumtafuta utampata tu na wala hutotumia nguvu kubwa sana kumpata, ndege wa rangi moja huruka pamoja, kwa jinsi maisha yako yalivyo James kwa sasa, huwezi kuwa na mwanamke kama Carry, hilo sahau."

"Sawa, nimekuelewa." Akaongea kwa kushusha pumzi kubwa kama mtu aliyetoka kukimbia mbio ndefu za marathon."

"Sasa usiondoke bila kula chakula cha mchana kabisa."

"Aaah, dada wewe ndiyo ninachokupendea, umekuwa mwokozi wangu sana..."

"Usijali kuhusu hilo, nimepika wali na njegere, unakula?" Swali hilo lilimfanya James aangue kicheko

"Dada wewe, kwa hali niliyonayo kuna chakula ambacho nitachagua mimi."

"Haya subiri kwanza ule ndiyo uondoke."

********************************

Wiki mbili baadaye James alirejea katika hali yake ya kwaida. Alipona kabisa na akaenda tena kupima kwa msaada wa pesa za Carry na hakuwa tena na magonjwa yaliyokuwa yanamsumbua malaria na UTI.

Hakutaka kuonekana si mkarimu kwa kutoweka tu au kutokwenda kutoa shukrani sehemu ambayo alipata msaada.

Alipofika kama kawaida aligonga geti, kwa bahati mbaya au nzuri lilifunguliwa na Catty.

"Hivi wewe kaka, kudowea kwenye nyumba za watu utaacha lini? Maana sasa ushazoea, asubuhi upo, mchana hukosekani, jioni ikifika huyu hapa, we vipi? Yaani sisi wanawake wazima tukulishe, wewe unajua pesa sisi tunapata wapi?"

"Sijaja kula leo!" Akajibu.

"Umemfuata Catty? Sasa hivi umehamia kwa mdogo wangu? Hakutaki babu we, yaani unavyoona amekulipia pesa ya matibabu na kukupa chakula wiki zote hizi mbili, sijui tatu basi unaona unapeeendwa!"

"Sijamfuata Catty, nimemfuata Carry!" Akamzingua.

"Umegonga mwamba kwa Carolina sasa unamtaka nduguye Catherine, na umasikini huo, tukupeleke wapi?"

"Carry unaongea na nani wewe huko?" Sauti ikasikika toka ndani. Ilikuwa ya mdogo wake.

Hakujibiwa kitu na James alikuwa amenyamaza kimya akiwa anaangaliana na Carry kama majogoo.

Baada kuona hajibiwi, Catty alijiongeza, akatoka ndani kuangalia kuna tatizo gani.

Kwa hali aliyoikuta alijua nini kitaendelea. Hakutaka kuuliza kitu.

"Karibu James, karibu mgeni wangu!" Akamkaribisha na kumfanya James kupata nguvu ya kumtambuka Carry, akaingia ndani.

Tayari alikuwa ameshapazoea, alikwenda moja kwa moja kwenye kochi. Akachukua rimoti mwenyewe, akaweka flashi kwenye TV na kuwasha kuangalia filamu anayoipenda.

Catty aliamua kumuacha kwanza aendelee na kuangalia TV, lakini James alimwita.

"Da' Catty, samahani nakuomba kidogo leo sikai sana."

> **"Unaenda wapi tena mwanaume wewe, umeshapona unaanza hivyo," akatania.**

"Unaenda wapi tena mwanaume wewe, umeshapona unaanza hivyo," akatania.

James aliangua kicheko, halafu kikamalizika kwa kumjibu," hapana leo nimepata tenda, kibarua cha kumsaidia fundi kujenga Tandale. Kuna ukuta wa mtu umebomoka huko.

"Umeshapona sawasawa, lakini hadi unaanza kufanya kazi, au unaharakisha kwa sababu huna pesa?"

"Hapana dada yangu, nimeshapona. Ile ile wiki ya kwanza na nusu nilikuwa nimeshapona, nikakaa kwanza kusikilizia naona kila siku nguvu zinarudi na niko fiti sasa kama zamani."

Catty alikaa kwenye kochi karibu na James ili kumsikiliza alichotaka kumwambia.

"Kiasi cha wiki mbili na ushehe ni kama nilikuwa naishi hapa. Nimehudumiwa, kwa chakula tangu asubuhi, mchana na usiku, nimepatiwa pesa ya matibabu na hata ya kutumia. Nashukuru sana kwa wema wote ulionifanyia. Leo naomba kukuaga. Narudia kwenye maisha yangu ya kawaida, sitokusahau maisha yangu yote."

Catty alishusha pumzi ndefu. Halafu akajibu kwa sauti ndogo ya huzuni, "Usijali James, kama unajiona unaweza kuendelea na maisha yako ya kawaida sawa, ila hapa tayari kumeshakuwa kwako, ukizungukazunguka uje kutuona na kutusalimia dada zako, hata sisi binadamu tunaweza tukawa na matatizo, tukaumwa, tukahitaji hata mtu wa kuja kumtuma soda tu dukani."

"Hakuna shida dada, nitaendelea na maisha yangu kama kawaida, lakini kwa mara kwa mara nitakuwa nakuja kuwasalimia. Ila nikimkuta Carry wewe haupo sasa halafu wewe haupo sijui itakuwaje?" Akasema na kuanza kucheka.

Catty akatabasamu na kumuuliza. "Vipi, umesahau? Si ndiyo itakuwa vizuri ili uendelee kumbembeleza?

Wote wawili waliangua kicheko.

Catty alianza kuona kama ushauri wake unaanza kumuingia kijana. James naye pia ilionekana alianza kuchoshwa na dharau na kejeli za Carry.

"Usihangaike na mtu asiyekupenda siku zote. Tafuta wa saizi yako. Usipende kudhalilishwa na kila mwanamke unayekutana naye barabarani." Akakumbuka maneno aliyoambiwa huko nyuma na Catty.

*Itaendelea Jumapili*



# TREVOR NOAH AWAKASIRISHA WAAFRIKA KUSINI

TANGAZO la dakika tano ambalo atashiriki mchekeshaji maarufu duniani, Emmy Trevor Noah, limeleta mpasuko nchini Afrika Kusini baada ya baadhi ya wabunge kupinga vikali.

Wabunge hao wanapinga kutumika kiasi kikubwa cha pesa zaidi ya randi milioni 33, sawa na shilingi bilioni 4 kama malipo yake.

Waziri wa Utalii wa Afrika Kusini, Patricia de Lille aliliambia bunge kuhusu mipango ya kumlipa Noah ili kushiriki katika video ya dakika tano inayotangaza utalii wa Afrika Kusini.

Wabunge wengi wamepinga pendekezo hilo, lakini De Lille anasema kuwa mcheshi huyo wa Afrika Kusini na mtangazaji wa TV hatalipwa kwa kutumia fedha za umma.

Alisema kuwa atalipwa kwa kutumia fedha za kibinafsi kutoka Baraza la Biashara la Utalii la Afrika Kusini, shirika ambalo linahusisha wadau wa usafiri na utalii wa nchi hiyo.

Baadhi ya raia wa nchi hiyo pia wamekosoa mpango huo kupitia mitandao ya kijamii wakisema haufai.

## *Msimdharau Mavoko kaokota fedha...*

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Rich Mavoko amejibu mashambulizi kutoka kwa mashabiki mbalimbali wanaosema kwamba amefulia, kuwa yeye anachokifanya ni kutafuta pesa hata ikiwa vijijini.

Hivi karibuni msanii huyo alisababisha mjadala baada ya kusambaa kwa video akionekana kuburudisha watu katika kiwanja kilichojaa vumbi.

"Nimepata pesa hata mkoba huwezi kuufunga, watu wasione masihara," amesikika akisema kwenye video ambayo anaonekana akiwa na waigizaji Tini White na Mkojani.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BRUNO, NEWCASTLE SAFI

KLABU ya Newcastle United imepiga hatua katika mazungumzo ya kurefusha mkataba wa kiungo wa Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 25 na makubaliano sasa yanaribia kufikiwa. ***(Fabrizio Romano)***

### CHELSEA, CITY VITANI

CHELSEA na Manchester City zilikuwa zinamfuatilia Bruno Guimaraes, ambaye mkataba wake wa Newcastle United utaendelea hadi ifikapo mwaka 2026. ***(90 min)***

### POTTER KUMRITHI BEALE

KLABU ya Rangers imemtaja kocha wa zamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter, kama mbadala wa kocha wa sasa, Michael Beale. ***(Football Insider)***

### NUSA ATAJWA ENGLAND

ARSENAL na Liverpool ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia winga wa Brugge kutoka Norway, Antonio Nusa, 18, ambaye alikataa nafasi ya kujiunga na Chelsea mwishoni mwa dirisha la usajili. ***(90mi)***

### TIEMEMANS MAMBO MAGUMU

KUKOSA muda wa kucheza kule Aston Villa kunamkwaza kiungo wa Ubelgiji, Youri Tielemans, 26, ambaye alijiunga na klabu hiyo kwa uhamisho wa bure msimu uliopita baada ya mkataba wake na Leicester City kumalizika. ***(Goal)***

### MITOMA KUULA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inapania kumsajili winga wa Japan, Kaoru Mitoma, 26, kwa mkataba mpya ifikapo mwisho wa mwaka. ***(90 min)***

### DE BEEK ANUKIA UTURUKI

KLABU ya Manchester United ingependa kumtoa kiungo wa kimataifa wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 26, kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa nchini Uturuki wiki ijayo. ***(Football Insider)***

### CHELSEA YAIBANIA WOLVES

CHELSEA iliingilia kati kuzuia Wolves kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa chini ya umri wa miaka 21, Habib Diarra (19) kutoka klabu 'dada' ya Strasbourg msimu huu. ***(Football Insider)***

### CARROLL ALITAKIWA EPL

MSHAMBULIAJI wa zamani wa England, Andy Carroll, 34, amesema alikuwa na ofa ya kubakia England kabla ya kuamua kujiunga na Amiens inayoshiriki Ligi 2 ya nchini Ufaransa. ***(Sun)***

### CHELSEA YAMSUBIRI LAVIA

KIUNGO wa Chelsea, Romeo Lavia (19) amepata jeraha la kifundo cha mguu wakati wa mazoezi na klabu hiyo inasubiri matokeo ya uchunguzi ili kubaini ukubwa wa jeraha lake kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji. ***(Guardian)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR AMPIKU PELE UFUNGAJI BORA BRAZIL

**AMAZON LA BELEM,** Bolivia

**Ni baada ya mshambuliaji huyo kufikisha mabao 79, mawili zaidi...**

NEYMAR amempita Pele na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa wanaume wa Brazil, akifunga mara mbili wakati timu yake ya taifa ikichapa Bolivia mabao 5-1 katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia iliyochezwa kwenye jiji la Amazon la Belém, juzi usiku.

**Fowadi huyo wa Al Hilal alifungana na Pele, ambaye aliifungia Brazil mabao 77 kati ya mwaka 1957 na 1971. Neymar sasa ana mabao 79 katika mechi 125 za kimataifa.**

"Sijawahi kufikiria kufikia rekodi hii. Nataka kusema mimi si mchezaji bora kuliko Pele," alisema Neymar baada ya mchezo huo.

"Siku zote nilitaka kutengeneza hadithi yangu mwenyewe, kuandika jina langu katika historia ya soka ya Brazil na timu ya taifa. Na leo (juzi) nilifanya hivyo."

Mshambuliaji wa kike wa Brazil, Marta anashikilia rekodi ya muda wote ya nchi hiyo akiwa na mabao 115 katika michezo 171 kwa timu ya taifa ya Wanawake.

Bao la kuvunja rekodi la Neymar lilipatikana baada ya krosi ndogo kwenye eneo la hatari, ambayo mshambuliaji huyo alimaliza kwa usahihi kwa shuti kali.

Mapema katika mechi hiyo, Neymar alikosa penalti dakika ya 17, ambayo kipa Guillermo Viscarra aliokoa.

Mfuko wa Hisani wa Pelé Foundation ulitoa maoni yake kwa mafanikio hayo ya Neymar.

"Hongera, Neymar Jr, kwa kumpita Mfalme kwa mabao ya Timu ya Taifa ya Brazil katika mechi rasmi za FIFA," ilisema taarifa hiyo kupitia kwenye mtandao wa kijamii. "Hakika Pele anakupongeza leo (juzi)!"

Pele alifariki kutokana na saratani Desemba 29, mwaka jana huko Sao Paulo akiwa na umri wa miaka 82.

Mshambulizi Rodrygo, ambaye pia alifunga mabao mawili dhidi ya Bolivia, alisema bado ni shabiki wa Neymar.

"Neymar ni shujaa wangu sana," alisema Rodrygo. "Hii itakuwa katika kumbukumbu yangu, hii ilikuwa siku ya kipekee sana."

Kocha mpya wa Brazil, Fernando Diniz alisema Neymar alikuja kuichezea Brazil "ili kufunga mabao, kuvunja rekodi, kuonyesha yuko tayari sana kuishi hivi na timu ya taifa."

"Yeye ni shujaa mkubwa," alisema Diniz. "Watu wanapaswa kumtambua na kumkubali."

Nyota huyo wa zamani wa Santos, Barcelona na Paris Saint-Germain alifunga bao lake la kwanza Brazil katika mchezo wa kirafiki mwaka 2010 dhidi ya Marekani.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI

FINLAND
VERSUS
DENMARK

1 | 5.49
X | 3.59
2 | 1.67

tigo pesa SportPesa

WASHINDI WA
MAOKOTO Deilee!

1. Adiedo John - 0652 251 XXX
2. Hamad Kasongo - 0653 199 XXX
3. Emanuel Jackson - 0654 406 XXX
4. Daniel Ngodola - 0672 096 XXX
5. Hafidhi Mawazo - 0711 823 XXX
6. James Shayo - 0714 900 XXX
7. Gerald Alphone - 0715 127 XXX
8. Rashidi Msisi - 0715 134 XXX
9. Edmund Yusto - 0717 650 XXX
10. Sielewi Chakal - 0718 624 XXX

20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WAARABU WA QATAR WAMNASA COUTINHO




**DOHA,** Qatar

PHILIPPE Coutinho ameondoka Aston Villa na kujiunga na Al-Duhail ya Qatar kwa mkopo wa msimu mzima.

Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 31 aliletwa Villa Park na kocha wa zamani, Steven Gerrard, tangu Januari, mwaka jana na mkataba wake wa awali wa muda mfupi kutoka Barcelona ukakamilika msimu uliofuata.

Lakini licha ya mwanzo mzuri wa kurejea Ligi Kuu England, mchezaji huyo wa zamani wa Liverpool ameshindwa kutimiza matarajio yake baada ya kusumbuliwa na kiwango duni na majeraha.

Coutinho alianza mechi saba pekee za ligi akiwa na Villa msimu uliopita, akifunga mara moja, huku akiuguza jeraha lingine la paja muda mfupi baada ya kutambulishwa dhidi ya Everton mwezi uliopita.

Baada ya kipindi kigumu tangu uhamisho wake wa pauni milioni 142 kwenda Camp Nou kutoka Liverpool mwaka 2018, sasa atatafuta kujenga upya soka lake Mashariki ya Kati.

Mchezaji huyo aliyeichezea Brazil mechi 68 bado ana miaka mitatu iliyosalia kwenye mkataba wake wa miaka minne aliosaini Villa msimu uliopita wa joto.




## Van Dijk aongezewa adhabu EPI

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool, Virgil van Dijk ameongezewa adhabu ya kufungiwa mchezo mmoja na faini ya pauni 100,000 baada ya kukubali mashtaka ya utovu wa nidhamu kwa mwamuzi, John Brooks kutokana na kuonyeshwa kadi nyekundu kwenye mechi dhidi ya Newcastle United.

Van Dijk alipewa onyo katika kipindi cha kwanza cha mchezo lakini faulo yake ilipokaguliwa na VAR, beki huyo wa Uholanzi alionekana akimtusi Brooks na kuelezea uamuzi huo kama "mzaha wa mfalme".

Adhabu ya kufungiwa mchezo mmoja kwa kadi nyekundu ya awali iliitolewa na Van Dijk akakosa kwenye mchezo wa ushindi wa 3-0 dhidi ya Aston Villa, lakini baada ya sauti ya kutoleana maneno na Brooks kuchunguzwa na Chama cha Soka cha England (FA), sasa amefungiwa mechi moja zaidi.

Taarifa ya FA ilise "Beki huyo alikiri alif mambo yasiyofaa na k mia maneno ya matus kwa afisa wa mechi ba ya kutolewa nje kwa nyekundu dakika ya 2 adhabu hiyo iliwekwa tume huru ya udhibiti.

"Sababu kamili ziliz dikwa za kesi hii zitach ishwa kwa wakati ufaa

Van Dijk sasa atakos fari ya Liverpool kuc dhidi ya Wolverhamp Wanderers Septemba mwaka huu.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# FOUNTAIN, RUVU SHOOTING HAPATOSHI CHAMPIONSHIP

**Na Abdallah Mataka**

MAAFANDE wa Ruvu Shooting wanatarajia kushuka ugenini kucheza dhidi ya Fountain Gate FC katika mechi ya Ligi ya NBC Championish itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani, Morogoro.

**Msimu mpya wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara ulianza rasmi jana.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Novatus Fulgence, alisema timu yake imejiandaa vizuri kuelekea kwenye mchezo huo na malengo yake ni kupambana na kupanda daraja.

"Kikubwa tumewaandaa wachezaji kisaikolojia, utimamu wa mwili kwa sababu tunaimani mwili unahitaji mapokeo mazuri ili kufanya vizuri zaidi katika mchezo huo unaotarajiwa kuwa mkali na wenye kuvutia," alisema Fulgence.

Aliongeza anatarajia kukutana na ushindani kwa sababu anakutana na timu yenye uzoefu wa michezo kwa kutokana na imetoka kushiriki Ligi Kuu Bara.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya KenGold itawakaribisha Transit Camp kutoka Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya jijini, Mbeya wakati Mbuni FC itakuwa mwenyeji wa Biashara United kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Raundi ya kwanza ya ligi hiyo itakamilika kesho kwa Pamba FC ya Mwanza itawaalika Mabingwa wa Fisrt League, Cosmopolitan kutoka Dar es Salaam ambayo imepanda daraja msimu huu.

Kocha Mkuu wa Pamba FC, Mbwana Makata, alisema kikosi chake kimejiandaa vyema kuhakikisha kinapata ushindi katika mechi hiyo ya kwanza.

"Tumejipanga vizuri, tutacheza kwa umakini na tahadhari, siku hizi hakuna timu ndogo, tutapambana kuhakikisha tunatumia vyema faida ya kucheza nyumbani," Makata alisema.

Bingwa na mshindi wa pili wa ligi hiyo watapanda moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu ujao wa 2024/2025 huku timu itakayomaliza katika nafasi ya tatu na nne zitacheza mechi za mchujo dhidi ya klabu za Ligi Kuu ambazo zitakuwa zimenusurika kushuka daraja moja kwa moja.

## Robertinho

INATOKA UK. 24

Kocha huyo aliongeza wapinzani wao wote (Kipanga, Cosmopolitan na Ngome FC), wamewasaidia kuongeza ubora katika kikosi chao na kufanya programu yake kabla ya kuivaa Power Dynamos iwe imekamilika.

Naye beki wa kulia wa timu hiyo, Shomari Kapombe alisema mechihizo za kirafiki walizocheza ilikuwa ni mipango ya Robertinho kupata muunganiko wa timu.

"Mechi hizi zimemsaidia Kocha Robertinho kupata muunganiko wa wale wa msimu uliopita na wapya, imesaidia kupata kombinesheni nzuri ndani ya timu. Amekuwa na malengo yake, sio kupata matokeo tu, bali ni kuona muunganiko wa timu," alisema Kapombe.

Aliongeza wanaendelea kujiimarisha kwa sababu katika mechi za kimataifa hakuna ugenini, wanahitaji kushinda mechi zote mbili.

Kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka nchini Alhamisi ili kuwafuata Power Dynamos kwa ajili ya mechi itakayochezwa Septemba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa ulioko Ndola.



Kocha Mkuu wa Namungo FC, Cedric Kaze (kulia), akimsikiliza kwa makini msaidizi wake, Denis Kitambi katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi za Ligi Kuu Bara itakayorejea kuanzia Septemba 15, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## *Yanga: Tumefunga hesabu*

INATOKA UK. 24

Wakati huo huo, Yanga imeendelea kutoa dozi baada ya kupata ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Kiluvya FC katika mechi ya kirafiki iliyofanyika kwenye Uwanja wa Avic Town ulioko Kigamboni jana.

Hafiz Konkoni na Kennedy Musonda kila mmoja amefunga mabao mawili katika mchezo huo wakati mengine yalipachikwa na Farid Mussa na Crispin Ngushi huku Maxi Nzengeli akitoa 'assist' ya tatu.

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 10/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4977 | Tokushima Vortis vs Iwaki FC | 2.97 | 3.17 | 2.18 |
| 13:30 | 5804 | Yenisey Kr vs Rodina Moscow | 2.57 | 3.17 | 2.47 |
| 14:00 | 2501 | Onsala BK vs Nassjo FF | 1.19 | 6.12 | 10.19 |
| 14:00 | 4834 | Yanbian Longding vs Jinan Xingzhou | 2.42 | 2.99 | 2.84 |
| 14:30 | 3708 | Dandong Tengyue vs Jiangxi Liansheng | 2.02 | 3.16 | 3.47 |
| 14:30 | 4546 | Shanghai Jiading Huilong vs Anhui Litian | 3.00 | 3.21 | 2.20 |
| 16:00 | 3398 | Kazakhstan vs Northern Ireland | 3.07 | 3.02 | 2.48 |
| 16:00 | 5043 | FC Futura vs Tips | 1.45 | 4.48 | 5.29 |
| 16:30 | 2917 | Thailand vs Iraq | 2.43 | 3.10 | 2.74 |
| 16:40 | 2310 | Ahli Al-Fujirah vs City Football Club | 1.39 | 4.33 | 6.25 |
| 17:00 | 1672 | Kozlovice FC vs Skastice | 1.67 | 3.88 | 4.08 |
| 17:00 | 3117 | Cibalia Vinkovci vs Solin | 1.73 | 3.38 | 4.24 |
| 17:15 | 2477 | Racing Ferrol vs Villarreal B | 1.90 | 3.22 | 3.96 |
| 17:15 | 3425 | Racing Santander vs Amorebieta | 1.82 | 3.28 | 4.27 |
| 17:30 | 1531 | Croatia Zmijavci vs NK Dubrava | 2.48 | 3.23 | 2.52 |
| 18:00 | 2465 | FC Alania Vladikavkaz vs FK Tyumen | 1.49 | 3.84 | 5.66 |
| 18:00 | 3089 | FK Mas Taborsko II vs Dukla Prague B | 2.27 | 3.54 | 2.58 |
| 18:00 | 4919 | Hostoun vs TJ Prestice | 2.33 | 3.54 | 2.51 |
| 18:00 | 5075 | Leningradets vs FC Dynamo Makhachkala | 2.98 | 2.98 | 2.28 |
| 18:00 | 5644 | Ourense CF vs Marino Luanco | 2.25 | 2.98 | 3.03 |
| 18:00 | 5973 | FC Hlinsko vs SK Benesov | 3.07 | 3.58 | 2.02 |
| 19:00 | 1019 | CD Covadonga vs Zamora CF | 3.28 | 3.03 | 2.11 |
| 19:00 | 1193 | Montenegro vs Bulgaria | 1.79 | 3.38 | 4.85 |
| 19:00 | 1678 | Faroe Islands vs Moldova | 2.44 | 3.05 | 3.10 |
| 19:00 | 4493 | Nigeria vs Sao Tome and Principe | 1.06 | 10.35 | 27.93 |
| 19:00 | 4821 | Finland vs Denmark | 5.49 | 3.59 | 1.67 |
| 19:00 | 4870 | Togo vs Cape Verde | 2.75 | 3.01 | 2.60 |
| 19:00 | 5917 | Hungary vs Czech Republic | 2.55 | 3.22 | 2.80 |
| 19:30 | 2235 | FC Cartagena vs Zaragoza | 2.97 | 2.92 | 2.43 |
| 19:30 | 2921 | Novara vs Pro Patria | 2.05 | 3.14 | 3.77 |
| 19:30 | 3135 | Mirandes vs FC Andorra | 3.03 | 3.03 | 2.33 |
| 19:30 | 5831 | Renate vs Pro Vercelli | 2.49 | 2.94 | 3.05 |
| 20:00 | 1741 | Espanyol B vs CF La Nucia | 2.42 | 2.92 | 2.82 |
| 20:00 | 3972 | Torrent CF vs CE Europa | 2.00 | 3.03 | 3.58 |
| 20:00 | 5389 | Linense vs Real Betis B | 1.74 | 3.22 | 4.43 |
| 20:30 | 2830 | Deportivo La Coruna vs CD Teruel | 1.31 | 4.40 | 9.20 |
| 20:30 | 3054 | Real Union Irun vs Rayo Majadahonda | 1.79 | 3.32 | 4.19 |
| 20:30 | 5314 | San Fernando CD vs Cordoba | 2.59 | 3.15 | 2.52 |
| 21:45 | 1757 | Lithuania vs Serbia | 8.92 | 5.31 | 1.32 |
| 21:45 | 1774 | Greece vs Gibraltar | 1.07 | 9.95 | 42.32 |
| 21:45 | 1803 | Ireland vs Netherlands | 5.05 | 3.74 | 1.68 |
| 21:45 | 2891 | Atletico GO vs Juventude RS | 1.99 | 3.08 | 3.67 |
| 21:45 | 3096 | San Marino vs Slovenia | 36.98 | 9.51 | 1.08 |
| 21:45 | 5394 | Albania vs Poland | 3.24 | 3.09 | 2.34 |
| 22:00 | 2598 | Valladolid vs Elche | 2.19 | 3.07 | 3.26 |
| 22:30 | 4072 | Guadeloupe vs Sint Maarten | 1.03 | 9.58 | 45.85 |
| 23:00 | 4257 | Sport Boys Association vs Sporting Cristal | 3.84 | 3.44 | 1.79 |
| 23:00 | 4537 | Martinique vs Curacao | 2.70 | 3.01 | 2.52 |
| 23:00 | 4995 | Chacaritas FC vs Vargas Torres | 2.00 | 2.94 | 3.85 |
| 23:30 | 5230 | Club Almagro vs Boca Juniors | 5.89 | 3.66 | 1.52 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Septemba 10, 2023

Nipashe




Neymar ampiku Pele ufungaji

UKURASA 21



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Kibu Denis (kushoto) na Mzamiru Yassin wakiwapungia mkono mashabiki waliojitokeza kuwapokea wakati kikosi hicho kikirejea nchini kikitokea Algeria jana alfajiri. Stars imefuzu kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON). **PICHA: TFF**

# Yanga: Tumefunga hesabu

## ●●● Yawaambia Al Merrikh hawataamini dozi watakayowapa katika...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI idadi kubwa ya mashabiki wamethibitisha watasafiri kuelekea Kigali, Rwanda kwa ajili ya kuishangilia Yanga, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi amesema kikosi chake kiko kamili na tayari kuwavaa Al Merrikh katika mchezo wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imefahamika.

**Al Merrikh ya Sudan itawakaribisha Yanga katika mechi ya kwanza ya hatua ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Septemba 16, mwaka huu kwenye uwanja wa Pele Nyamirambo ulioko nje kidogo ya Kigali.**

Waarabu hao wamechagua kutumia uwanja huo ili kujiepusha na hali ya machafuko yaliyoko Sudan kwa sasa.

Gamondi alisema ubora wa wachezaji wake umeongezeka na kalenda ya mapumziko ya kimataifa kwake ilikuwa na faida.

Kocha huyo alisema kwa sasa kila mchezaji anafahamu majukumu yake na wanaonyesha wanakiu ya kusaka matokeo chanya katika mechi hiyo ya kwanza ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele.

"Tuko tayari, tumefanya mazoezi yote muhimu kwa kuangalia mapungufu yaliyojitokeza katika mechi zilizotangulia, nimeona mabadiliko makubwa kwa kila mchezaji," alisema Gamondi.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Yanga, Ali Kamwe, alisema zaidi ya mabasi 26 yatakayobeba mashabiki yataondoka nchini na kuelekea Rwanda kwa lengo la kwenda kushuhudia mchezo huo. Kamwe alisema bado mashabiki wanaendelea kukata tiketi na kitendo hicho anaamini kitawashangaza wapinzani wao.

"Kuna mwitikio mkubwa wa mashabiki, wapinzani wetu Al Merrikh hawataamini watakachokishuhudia ndani na nje ya Uwanja wa Pele, Yanga inakwenda kuujaza uwanja huo na tumejipanga kucheza mpira mkubwa," alisema Kamwe.

Alisema mashabiki watakaokwenda Rwanda wanatoka katika mikoa ya Dar es Salaam, Shinyanga, Kigoma na Mwanza na kuongeza hali hiyo itawathibitishia wapinzani wao na Wanyarwanda namna Watanzania ni watu wanaopenda soka.

"Nakwambia mashabiki wa soka Rwanda, wapinzani wetu Al Merrikh nao hawataamini pale watakapoona msafara wa mabasi utakaoingia huko pamoja na kwenda kuujaza uwanja na hilo ndilo lengo letu kubwa, tutaujaza uwanja na kushangilia kama tupo nyumbani, na soka kubwa tutalionyesha," Kamwe alitamba.

Aliongeza baadhi ya wachezaji wa Yanga pia walitaka wasafiri kwa njia ya barabara na mashabiki wao lakini hilo haliwezekani kwa sababu za kiitifaki.

"Nimezungumza na wachezaji wetu (Dickson Job, Aboutwalib Mshery, Stephane Aziz Ki na Pacome Zouzoua, wao walitaka kusafiri na mabasi ya mashabiki wetu lakini haiwezekani kiprotokali, hivyo wamewaomba mashabiki wawashangilie kwa nguvu na wao watawalipa kwa kucheza soka safi na kupata ushindi ugenini kwa ajili ya kurahisisha kazi nyumbani," alisema ofisa huyo.

Baada ya mechi hiyo ya Jumamosi, Yanga itarejea nyumbani na kuwasubiri Wasudan hao kwa ajili ya mchezo wa marudiano utakaochezwa Septemba 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

INAENDELEA UK. 23

# Robertinho atamba kitaumana Zambia

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kupata michezo mitatu ya kirafiki, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' amesema sasa anaridhishwa na safu yake ya ushambuliaji kwa sababu kila mchezaji anayecheza nafasi hiyo anatekeleza majukumu yake vyema.

Katika michezo hiyo, Jean Baleke, Willy Essomba Onana na Aubin Kramo, walifanikiwa kuonyesha kiwango kizuri na kufunga mabao ambapo katika mechi ya jana asubuhi Wekundu wa Msimbazi waliibuka na ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Ngome FC.

Mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena Dar es Salaam ilikamilisha michezo mitatu ya kirafiki kabla ya kuelekea Zambia katika mchezo wao wa hatua ya pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji Power Dynamos.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo ya mazoezi, Robertinho alisema katika mechi hizo tatu walizocheza washambuliaji wake wote wamefanikiwa kufunga mabao jambo linalompa matumaini makubwa kuelekea mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Robertinho alisema pia kila mchezaji ameimarika na kuonyesha yuko tayari kwa mapambano kwa sababu wanahitaji kufikia malengo.

"Mchezo ulikuwa mzuri, nimefurahishwa na kiwango cha wachezaji wangu na kupata ushindi katika michezo yote mitatu. Huu utakuwa mchezo wa mwisho wa kirafiki, sasa rasmi tunaingia kwenye mipango ya kuikabili Power Dynamos," alisema Robertinho.

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >